**WALIMU** matatani kwa tuhuma za kujihusisha mapenzi na wanafunzi

UKURASA 16



**SERIKALI** yapata mwarobaini upungufu mafuta ya kula

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Mei 10, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580576

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# MOSHI MWEUPE

**AJIRA** maelfu alizoahidi Samia zatangazwa, waombaji lazima wawe na namba ya NIDA... *Endelea Ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan, akitoa heshima za mwisho kwenye Jeneza lenye mwili wa Marehemu Teddy Mapunda, katika viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

### RAIS AMKABIDHI KIKWETE NYUMBA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemkabidhi nyumba ya kuishi Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, iliyojengwa katika Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam...

**UKURASA WA 3**

### MWILI ULIOZUIWA KCMC WAZIKWA

HATIMAYE mwili wa Bauda Nkya (68), aliyefariki dunia siku tisa zilizopita na mwili wake kudaiwa kuzuiwa katika Hospitali ya Rufani ya KCMC ili kulipa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 3.5, umezikwa kijijini kwao Kitongoji cha Muro-Nshara wilayani...

## Samia aongoza mazishi ya Teddy

UKURASA 3

**RIPOTI MAALUM**

## Utukutu shule sekondari waweka wanafunzi, walimu kwenye hofu

UKURASA 4

**MICHEZO** SIMBA, YANGA KUKIMBIANA NDIZO ZAO, HAIKUANZA J'MOSI UK. 14

MAONI, KATUNI UK. 6

# Moshi mweupe ajira serikalini

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MOSHI mweupe! Ndivyo unavyoweza kusema, baada ya serikali kutoa kibali cha ajira mpya 9,675 za walimu wa shule za msingi, sekondari na watumishi wa kada za afya huku ikiwataka waombaji wa ajira hizo kuwa na namba ya kitambulisho cha taifa.

Maombi ya ajira yalianza jana kwa njia ya mtandao hadi Mei 23 mwaka huu ambapo kwa upande wa walimu, kibali kimetoka kwa ajira ni 6,949 na afya ni 2,726.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alisema jana ajira hizo zitajaza nafasi zilizoachwa wazi na watumishi waliokoma utumish. "Serikali imetoa kibali, maana mara baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kueleza kwamba atatoa ajira 6,000 kwa walimu, tulikuwa tunapata msukumo mkubwa kutoka kwa wananchi wakihoji kwanini TAMISEMI hatutangazi, taratibu za serikali lazima tupate kibali Menejimenti ya Utumishi wa Umma," alisema.

Ummy alisema taratibu zote za uombaji wa ajira hizo umekamilika na wale wote wenye nia ya kuomba ajira, wataomba kupitia kiunganishi cha ajira.tamisemi.go.tz kuanzia jana.

Hata hivyo, alisema serikali imetoa fursa kwa waombaji ambao wana ulemavu kutuma maombi yao kwa nakala ngumu na yaeleze aina ya ulemavu wao na picha zao na kutumwa kwa anuani ya Katibu Mkuu TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu ili aione Mkurugenzi wa Kitengo cha Watu Wenye Ulemavu.

**SIFA ZA UALIMU**

Akitaja sifa za waombaji wa ualimu, Waziri Ummy alisema kwa shule ya msingi, wanatakiwa walimu wenye daraja la IIIA kuwa astashahada ya elimu ya msingi, elimu ya michezo, elimu ya awali na elimu maalum.

"Mwalimu wa daraja la IIIB anatakiwa kuwa mhitimu wa stashahada ya ualimu wa elimu ya awali, msingi, elimu maalum na mwalimu wa daraja la IIIC, mhitimu wa shahada ya ualimu masomo ya lugha ya Kiingereza, Historia na Jiografia," alisema.

Alisema kwa shule za sekondari wako kwenye makundi manne ambayo ni mwalimu wa daraja IIIB ambao wamehitimu stashahada ya ualimu wa masomo ya Fizikia, Hesabu, Baiolojia na Kemia.

"Pia mwalimu wa daraja IIIC ambaye amehitimu ualimu aliyesomea elimu maalum kwa masomo hayo na shahada ya ualimu wa masomo hayo, pia awe amehitimu stashahada ya uzamili katika elimu, lazima awe mwenye shahada ya kwanza yenye masomo tajwa," alisema.

**WALIOSOMEA NJE YA NCHI**

Waziri Ummy alisema kwa waombaji wa ajira hizo ambao wamesoma elimu ya sekondari nje ya nchi, wanatakiwa kupata namba ya ulinganifu wa matokeo inayoanzia na herufi EQ... kutoka Baraza la Mitihani (NECTA) ili kuingia kwenye mfumo wa maombi ya ajira.

"Pia wanatakiwa kupata ithibati ya masomo yao kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU), ili vyeti vyao vitambulike na kupata uhalali wa kutumika nchini,"alisema.

**SEKTA YA AFYA**

Ummy alisema kada za afya ambazo serikali itaajiri ni daktari daraja la II, daktari wa meno daraja la II, tabibu daraja la II, tabibu msaidizi, tabibu wa meno daraja la II, tabibu wa meno msaidizi na mfamasia daraja la II.

Nyingine ni mteknolojia wa dawa daraja la II, mteknolojia msaidizi wa dawa, mteknolojia wa maabara daraja II, mteknolojia msaidizi maabara, mteknolojia mionzi daraja la II, mteknolojia msaidizi wa mionzi na mteknolojia wa macho daraja la II.

Alisema serikali itaajiri ofisa muuguzi daraja la II, ofisa muuguzi msaidizi daraja la II, muuguzi daraja la II, mtoa tiba kwa vitendo daraja la II, ofisa afya mazingira daraja la II, ofisa afya mazingira msaidizi daraja la II, msaidizi wa afya, katibu wa afya daraja la II, ofisa ustawi wa jamii daraja la II na ofisa lishe daraja la II.

**NAMBA YA NIDA**

Akitoa ufafanuzi wa kuhusu ulazima wa kuwa na namba ya NIDA, Waziri Ummy alisema sekretarieti ya ajira imetoa maelekezo kuwa ni lazima mwombaji kuwa na namba hiyo.

Waziri huyo alisisitiza waombaji wawe tayari kufanya kazi kwenye halmashauri walizopangiwa na hakutakuwa na nafasi ya kubadilisha kituo cha kazi.

## Rais Samia amkabidhi JK nyumba

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemkabidhi nyumba ya kuishi Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, iliyojengwa katika Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam.

Nyumba hiyo imejengwa na Serikali ya Tanzania kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ikiwa ni utekelezaji wa kifungu namba 12 cha Sheria ya mafao ya hitimisho la kazi kwa viongozi wa siasa, sura ya 225 na marejeo ya mwaka 2020 ambayo pamoja na stahili zingine za matunzo ya viongozi wakuu wastaafu inaelekeza kuwa Rais anayestaafu anastahili kujengewa nyumba ya kuishi yenye hadhi ya Rais.

Akizungumza baada ya kukabidhi nyumba hiyo jana, Rais Samia alimpongeza Rais Mstaafu Kikwete kwa kupata makazi hayo na amemhakikishia kuwa serikali itaendelea kumtunza yeye na viongozi wengine wastaafu kama inavyoelekezwa katika sheria.

Alibainisha kuwa serikali itafanyia kazi uboreshaji wa sheria hiyo pamoja na kuhakikisha wajane/wagane wa viongozi wanatunzwa.

Rais Samia alimuagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Mohamed Mchengerwa, kuanza maandalizi ya kutimiza haki zote anazostahili aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Kwa upande wake, Waziri Mchengerwa alisema nyumba hiyo ni ya 3 kukabidhiwa ikitanguliwa na nyumba ya Rais Mstaafu, Hayati Benjamin Mkapa na Rais Mstaafu, Dk. Ali Hassan Mwinyi, na kwamba nyumba ya Baba wa Taifa, Hayati Julius Nyerere ilijengwa na kukabidhiwa kwake na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Dk. Jakaya Mrisho Kikwete aliyeongozana na mkewe, Mama Salma Kikwete, aliishukuru serikali kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kutekeleza takwa hilo la kisheria, aliishukuru TBA kwa kukamilisha ujenzi tangu ulipoanza mwaka 2018 na alimshukuru Rais Samia kwa kumkabidhi nyumba hiyo.



Wafanyakazi wa kampuni ya The Guardian Ltd wakipata futari iliyoandaliwa na kampuni hiyo Mikocheni jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi yapiga marufuku maandamano ya BAWACHA

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma, limetoa onyo kwa Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) wanaoshawishi kufanya maandamano yasiyo na kikomo nchi nzima husussani Mkoa wa Dodoma kusitisha mara moja.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alitangaza marufuku hiyo jana jijini Dodoma, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Kamanda Muroto alisema kuwa maandamano hayo ni haramu na yanatakiwa kupuuzwa na wananchi wote.

"Ni marufuku na hayakubariki kwa mujibu wa K/F 43 (1) (a) (b), (3) (4) na K/F 44 cha sheria ya huduma za polisi na polisi wasaidizi sura ya 322 maandamano hayo yana viashiria vya uvunjifu wa amani kwa kuwa hayana malengo maalum wala ukomo," alisema Kamanda Muroto.

Aidha, alisema Mkoa wa Dodoma hakuna nafasi ya maandamano hayo na kila mtu awajibike katika kazi zake halali za maendeleo wala wasidanganyike na watu wanaotafuta umaarufu kwa kuhamasisha uhalifu.

"Asiyefunzwa na mamaye atafunzwa na Kamanda wa polisi Dodoma, wajiaandae kuja na madaftari (counter book kwaya 5) au computer ili wakirudi kwao wakafundishe wenzao watakachokipata Dodoma.

"Wajiandae kuja na bukta za kukimbia masafa mafupi sisi tumewaandalia maji ya kuoga baada ya masafa hayo mafupi na watachagua maji ya moto au ya baridi," alisema Kamanda Muroto

Hivi karibuni chama cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA kupitia BAWACHA Taifa kilitangaza kufanya maandamano ya amani kuanzia wilayani Kongwa mkoani Dodoma, kushinikiza Spika wa Bunge, Job Ndugai, awaondoe wabunge 19, bungeni waliovuliwa uwanachama.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kati, Aisha Luja, alisema wanatarajia hivi karibuni kufanya maandamano ya amani kuanzia wilayani Kongwa lengo likiwa ni kushinikiza Spika Ndugai awaondoe wabunge hao bungeni.

Alisema kuwa Ili wapate haki yao watafanya maandamano ya amani kuanzia wilayani Kongwa.

"Ni vema Spika Ndugai kutumia vifungu vya sheria na kanuni alivyotumia kumuengua Sofia Simba, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum baada ya kufukuzwa uanachama na chama chake CCM pamoja na wabunge 8, wa CUF, azitumie sheria hizo katika kutenda haki,"alisema

## HABARI KITAIFA

# Serikali yapata mwarobaini upungufu mafuta ya kula

**Na Hellen Mwango**

WAKATI nchi ikikabiliwa na uhaba wa mafuta ya kula na bei kupanda kwa kasi, serikali imesema itafanya mchakato wa muda mfupi kukabiliana na tatizo la uhaba wa mafuta nchini.

Aidha, imesema upungufu wa bidhaa hiyo unatokana na viwanda vya mafuta nchini kufungwa kutokana na kodi ya mafuta ghafi kuwa juu.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Mkumbo, wakati akizungumza na wafanyabiashara wa mafuta.

“Sisi kama serikali tuna matarajio ya muda mfupi kwamba ndani ya miezi miwili ijayo tukianza kuvuna zao la alizeti bei ya mafuta itashuka,” alisema na kuongeza:

“Kwa sasa wafanyabiashara wanalazimika kuagiza mafuta ya mawese yaliyochakatwa kutoka nje na gharama yake awali ilikuwa Dola za Marekani 600, lakini imepanda mpaka Dola 1,200 kwa sababu viwanda vyetu hapa nchini vilivyokuwa vinachakata mafuta havifanyi kazi.”

Akifafanua kuhusu kufungwa kwa viwanda vitatu vya kuchakata mafuta nchini, Prof. Mkumbo alisema vimeshindwa kuendelea kufanya kazi kwa sababu ya ‘ujanjaujanja’ mwingi.

“Wafanyabiashara walikuwa wanasema wanachakata mafuta kutoka ndani ya nchi wakati walipata kutoka nje ya Tanzania,” alisema.

Hata hivyo, amewaagiza wafanyabiashara hao kwenda kuandaa hoja ili ziwasilishwe kwenye mchakato ikiwamo kubadilisha gharama za kodi wanazolalamikia kutoka asilimia 25 kurudi asilimia sifuri kama ilivyo kwa nchi za Afrika Mashariki.

Pia, akizungumzia zao la alizeti, waziri alisema kwa sasa nguvu zielekezwe kwenye kilimo cha zao hilo kwa sababu mpaka kufikia 2022, Serikali itakuwa imefanikiwa kupata mbegu bora itayozalisha kwa wingi na kukidhi hitaji, na kwamba kwa sasa zinahitajika tani 500,070 za bidhaa hiyo.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao, Gulam Dewji, alisema Serikali ilipandisha kodi ya mafuta ghafi kutoka asilimia sifuri mpaka 25, hali iliyokwamisha uzalishaji wa ndani.

Alisema kampuni yake ya Mohamed Enterprises Tanzania Limited (METL) Group inazalisha zaidi ya tani 2,000 kwa siku, lakini kutokana na soko la dunia kuongezeka kutoka Dola za Marekani 600 mpaka 1,200, wanalazimika kuendana na gharama hizo.

“Bei ya mafuta imepanda mara mbili katika soko la dunia, bado asilimia 60 ya mafuta yanatoka nje kuingia hapa nyumbani hatuna mafuta ghafi nchini, tumezungumza na waziri amekubali kulifanyia kazi suala la kodi kurudi asilimia sifuri,” alisema Dewji.

Alisema kodi ikishuka, soko la mafuta litarudi nchini na watasambaza na nchi jirani kama ilivyokuwa awali.

Naye mfanyabiashara Fuad Awadhi wa Azania Oil, alisema ajira zaidi ya 10,000 za Watanzania zimepotea kutokana na viwanda vya mafuta kufungwa nchini kwa sababu ya kiwango kikubwa cha kodi.

Alisema hata kama wakulima wanalima zao la mchikichi, viwanda vimebaki magofu, havifanyi kazi hasara itakuwa kubwa kwao wote.

# Mwili uliozuiwa KCMC wazikwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

HATIMAYE mwili wa Bauda Nkya (68), aliyefariki dunia siku tisa zilizopita na mwili wake kudaiwa kuzuiwa katika Hospitali ya Rufani ya KCMC ili kulipa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 3.5, umezikwa kijijini kwao Kitongoji cha Muro-Nshara, wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro.

Mwili huo uliondolewa jana asubuhi KCMC baada ya familia kukamilisha taratibu za kulipa gharama hizo.

Mwili wa Bauda ulizikwa jana majira ya saa saba mchana baada ya swala ya adhuhuri katika makaburi ya familia yake huko Kitongoji cha Muro, Kijiji cha Nshara, Machame Kaskazini, Wilaya ya Hai.

Juzi, Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, alipokwenda kuwapa pole wafiwa na kuzungumza na familia hiyo, ambayo ni miongoni mwa kaya zinazohudumiwa na Mfuko Maendeleo ya Jamii (TASAF), alisema serikali imeliona jambo hilo na imeamua kubeba mzigo huo wa gharama.

“Nimekuja kuwapa pole kwa msiba huu. Serikali imekisikia kilio chenu na kuiona huzuni yenu na uchumi mlio nao. Niahidi hapa kwamba tutalisimamia jambo hili msihuzunike.

“Ofisi yangu kupitia DAS (Katibu Tawala wa Wilaya), Upendo Wella, itabeba jukumu hilo la malipo kutokana na uduni wa familia hii.

“Kimsingi, hii familia ni duni na ukitazama kabisa haina uwezo wa kulipa Sh. milioni 3.5, huo ni miujiza.

“Kwa hiyo anzeni maandalizi ya kuzika, ofisi yangu kupitia kwa DAS itafanya mawasiliano na huu mwili utaletwa kesho (jana) nyumbani kuzikwa,” alisema.

Bibi huyo alifariki dunia Mei 2, mwaka huu kutokana na kile kilichoelezwa na familia kuwa alijikwaa kwenye kisiki na kupata jeraha sehemu ya mguu ambalo lilisababisha mguu kuoza.

Akizungumzia kifo cha mama yake, mtoto wa marehemu, Muzaimata Urassa, alisema baada ya mama yao kufariki dunia katika Hospitali ya Rufani ya KCMC, walipewa taarifa ya gharama hiyo ya Sh. milioni 3.5.

Alisema kwa siku kadhaa wamekuwa wakiomba kuchukua mwili wa mama yao, baada ya kupunguza gharama hiyo kwa kupeleka kiasi Sh. milioni 1.1 lakini hawakukubaliwa kuchukua mwili.

Hata hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa KCMC, Profesa Gileard Masenga, alisema hakuwa na taarifa hiyo alipoulizwa na Nipashe juzi.

# Samia aongoza mazishi ya Teddy Mapunda

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana, aliwaongoza waombolezaji, jijini Dar es Salaam katika mazishi ya kumuaga aliyekuwa Mkurugenzi wa kampuni ya Montage, Teddy Mapunda, aliyefariki dunia Mei 4, mwaka huu.

Mazishi hayo yaliyofanyika kwenye viwanja vya Karimjee, pia yalihudhuriwa na Rais Mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete na viongozi wengine akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Aboubakar Kunenge.

Awali akiongoza ibada ya mazishi, Paroko Joseph Matumaini wa Parokia ya Mtakatifu Joseph, jijini Dar es Salaam, alisema Teddy ameacha alama kwenye jamii kwa kuwa alitoa mchango mkubwa katika kanisa na kwa watu wenye uhitaji maalum, wakiwamo yatima.

Paroko Matumaini alisema wakati waombolezaji wakimuaga Teddy, watambue kwamba siku ya kifo cha binadamu haijulikani, hivyo ni vyema kuishi maisha mema kwa ajili ya wengine.

“Kuna maisha baada ya kifo... katika kanisa tunaamini ni duniani na mbinguni, tumuombe Mungu katika siku ya leo, isiwe kama destruri ya kusindikiza, bali tujiandae.

“Wapo wanaojiuliza kwamba binadamu afe akiwa na umri gani, labda awe mzee, kwamba akifa kijana ni mapema sana. Lakini kristo alikufa akiwa na umri wa miaka 32.

“Jambo la maana duniani si muda mrefu wala mfupi, bali ni kwa ajili ya ulimwengu. Maisha si kwa ajili yetu binafsi, bali ni kwa wengine,” alisema Paroko Matumaini.

Aidha, mtoto wa marehemu, Telvin Mapunda, akisoma wasifu wa mama yake, alisema alizaliwa Januari 21 mwaka 1975 jijini Dar es Salaam.

Alisema mama yake alipata elimu ya sekondari katika Shule Jangwani hadi kufika chuo kikuu kilichopo Uingereza na baadae kwenda kuendelea na masomo Scandnavia na kupata Shahada ya Biashara na mauzo na alikuwa mtaalamu wa masuala ya uhusiano wa ndani na nje ya taasisi.

Telvin alisema mama yake aliwahi kufanya kazi kama mkurugenzi wa kampuni ya Serengeti na baadae kufugua kampuni yake ya Montage, ambayo inajihusisha na uandaaji wa matukio tofauti, dhifa na sherehe mbalimbali.

“Mama alikuwa akitoa msaada kwa yatima, kutoa elimu ya kufanya biashara kwa vijana na aliajiri vijana 40 kwenye kampuni yake.” alisema Telvin na kuongeza:

“Mama alijisikia vibaya akiwa katika futari aliyoandaa na alifariki saa 5:10 usiku baada ya moyo kusimama ghafla na pia kwa ugonjwa wa kisukari.”

Mkurugenzi wa Masoko kutoka Bodi ya Utalii Tanzania, Mindi Kasiga, alisema kwa niaba ya taasisi nyingine, Teddy atakumbukwa katika kukuza utalii nchini.

Teddy Mapunda, alifariki dunia Mei 4, mwaka huu, baada ya kujisikia vibaya akiwa na rafiki zake katika Hoteli ya Serena, kwa wa mujibu wa rafiki zake wa karibu, alikimbizwa katika hospitali ya Aga Khan kwa ajili ya matibabu, ingawa baadaye ilielezwa amefariki dunia.

Mwili wake unatarajiwa kuzikwa leo mkoani Dar es Salaam.



RIPOTI MAALUM

# Utukutu shule sekondari waweka wanafunzi, walimu kwenye hofu

**Na Yasmine Protace**



Prof. Ndalichako, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

UTUKUTU unaodaiwa kukithiri katika Shule ya Sekondari Misitu, iliyopo wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam, umesababisha shule hiyo kugeuka eneo la hatari kwa wanafunzi wanyonge na walimu.

Pia, inadaiwa kuwa uvutaji bangi na madawa ya kulevya umekithiri huku vijana wahuni wakihusishwa kufanya urafiki na wanafunzi na kushiriki kwenye vitendo hivyo viovu.

Imedaiwa kuwa wanafunzi kwenda shuleni na silaha za jadi kama mapanga, visu, bisibisi na viwembe ni jambo la kawaida na kutumika kuwajeruhi wanafunzi wanyonge na walimu.

Baadhi ya matukio yaliyoripotiwa ni mwanafunzi kumchana kwa wembe mwanafunzi mwenzake na kuvunjwa mkono, kukabana na kuibiana vifaa vya shule.

Walimu ambao hawakutaka kutajwa majina yao gazetini, wamedai kuwa matukio hayo ni tishio kwa usalama wao, wanafunzi na wafanyakazi wengine shuleni hapo.

Wamedai vitendo vya wanafunzi wa kiume kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi wa kike ni jambo la kawaida na wakati mwingine kupigana bila woga wanapochukuliana wapenzi.

Mwanafunzi Rahmu Simba wa kidato cha nne ni mmoja wa waathirika wa matukio ya utukutu kwa kuchanwa kwa wembe mkononi na kushonwa nyuzi saba.

Mmoja wa walimu, aliiambia Nipashe kuwa Rahmu alichanjwa kwa wembe baada ya kukataa kumpa pesa mwanafunzi mwenzake.

Alisema tukio hilo lilisababisha watuhumiwa kukamatwa na kufikishwa Kituo cha Polisi Stakishari, lakini waliachiwa kwa dhamana baada ya kukaa siku tatu ndani na kurudi shuleni, jambo alilodai linatishia usalama wa wanafunzi wengine.

Mwanafunzi aliyejeruhiwa alifunguliwa jalada namba STK/RB/1698/2021 na baada ya tukio hilo mzazi wake alikwenda kumchukua.

Kwa mujibu wa mwalimu huyo, mwanafunzi mwingine wa kidato cha tatu, Abdallah Idd, alivunjwa mkono kwa kuvamiwa na wahuni wakati akienda chooni na taarifa zilipelekwa kwa Ofisa Elimu Sekondari na mzazi wake.

Alisema tatizo la shule kukithiri vitendo hivyo ni kutokuwa na uzio, licha ya kuwa na walinzi, utukutu wa wanafunzi umekithiri na wanakuja na mbinu mpya kila siku.

Licha ya matukio hayo, mwalimu huyo alisema wanafunzi hao waliotuhumiwa kufanya vitendo hivyo wameendelea na masomo kama kawaida na uongozi wa shule uliwasamehe, jambo ambalo limechochea utukutu.

"Unakuta mwanafunzi au wanafunzi wanafanya makosa makubwa au ya kawaida, hatutakiwi kuchukulia hatua, vitendo hivyo vinachangia wanafunzi kuzidi kuwa sugu," alisema.

**MKUU WA SHULE**

Mkuu wa Shule hiyo, Anna Gale, alipoulizwa kuhusu madai hayo, alisema matukio hayo yanafanyika nje ya shule, ambako usimamizi unakuwa ni wa wazazi.

Hata hivyo, alisema hajapokea taarifa zozote za wanafunzi wake kuvuta bangi au kwenda na silaha shuleni.

Pia, alisema hajapokea taarifa za wanafunzi kuporwa mabegi au kukabana wala wanafunzi kuvunjwa mkono au kuchanwa wembe.

Alifafanua kuwa tukio la mwanafunzi kuvunjwa mkono na mwingine kuchanwa kwa wembe halikutokea eneo la shule hiyo, taarifa alizonazo yalitokea kwenye daladala.

"Matukio yanayotokea nje ya shule hatuwezi kuyazungumzia, akiwa shuleni ni mwanafunzi wetu, lakini akiwa nje ni wajibu wazazi na jamii," alisema.

**MRATIBU ELIMU AFUNGUKA**

Mratibu wa Elimu kata ya Kivule, Urumbi Kitila, alisema malezi duni ndio chanzo cha watoto kuharibika na kwamba wanafunzi hubeba silaha za jadi kama sime, nyembe kwa ajili ya kushambulia wenzao.

"Watoto wanatoka nyumbani wazazi hawana utaratibu wa kukagua mabegi yao na hivyo watoto kubeba sime, nyembe, visu na kuingia navyo shuleni.

Hata tukiwaita wazazi kwenye vikao vya shule hawaji," alisema.

Kwa mujibu wa Kitila, watoto wanapokuwa na vitu vya hatari katika mabegi yao, hutumia vifaa hivyo wanapokuwa nje ya shule au vipindi vikiwa vinaendelea.

Alisema wapo wanafunzi wa kike na wa kiume wa shule hiyo masomo yanapoendelea wao wanakuwa katika makazi ya watu wamekaa, jambo linaloonesha kuwa hata jamii inayozunguka shule haina mwamko wa elimu.

"Nimekuwa nikiwafukuza, pamoja na kuwafukuza wanatoa maneno yasiyofaa," alisema.

Alisema ofisi yake ipo jirani na shule na hata dirisha la ofisi yake limeangalia eneo ambalo watoto wanapita na kuwafuatilia, anapowakanya wanamtolea maneno mazito hali inayomkatisha tamaa na kuamua kuwaacha.

Hata hivyo, alisema ofisi yake ilichukua hatua kuwadhibiti wanafunzi wanaotoka eneo la shule huku vipindi vikiendelea kwa kuweka mgambo wa kuwazuia.

Alisema hali ya utoro ilianza kutulia, lakini mgambo walipoondoka, hali ilirudi na fujo za kutoka darasani zinaendelea.

Ofisa Elimu Sekondari Ilala, Mussa Ally Musa, aliiambia Nipashe kuwa tatizo hilo halipo kwenye shule ya Misitu pekee, wanapata taarifa kutoka kwenye shule nyingine pia na kutatua.

Alisema Ilala ina zaidi ya shule 100 za serikali na za watu binafsi, na kusisitiza ni wajibu wa wazazi kufuatilia nidhamu na maendeleo ya watoto wao badala ya kuwaachia walimu pekee.

"Nakumbuka kuna mzazi alikuja katika ofisi yangu na kunieleza kuwa kijana wake anasoma Misitu sekondari kavunjwa mkono, niliwashauri wazazi waendelee na matibabu na baadaye afike ofisini kwangu, lakini hakurudi," alisema.

Pia, alisema shule zote zina utaratibu mtoto anapoumizwa kamati zinawasikiliza na kama kutakuwa na ukubwa wa tatizo wanaenda polisi au wanamalizana na kamati za shule.

Pia, alisema kama mwanafunzi amefanya matukio nje ya shule, vyombo vya dola vinashughulikia mambo hayo, na kama kuna ushahidi wa kumjeruhi mwingine anafukuzwa shule.

Musa alisema kuna mkakati wa kuweka uzio katika Shule ya Sekondari Misitu na kuomba kibali kwa Mkuu wa Wilaya Ilala.

Alisema matukio kama hayo pia yalitokea katika Shule ya Sekodari Ulongoni na walibaini asilimia 80 ya wanafunzi wanavuta bangi, lakini waliwadhibiti kwa kuweka mgambo na polisi jamii ambao walipambana na wanafunzi hao katika magofu na walifanikiwa kuweka shule katika maeneo salama.

Ofisa Elimu huyo aliahidi kufika shuleni hapo kujua ukweli zaidi ili hatua zichukuliwe.

Meya wa Ilala, Omary Jumbilamoto, alisema zimetengwa Sh. bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika Shule ya Sekondari Misitu, ikiwamo ununuzi wa madawati katika shule zingine na ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule zingine.

Kadhalika, alisema ujenzi wa uzio huo utasaidia kupunguza matukio ya wahuni kuingia katika shule hiyo na wanafunzi kutulia darasani.

MAMA NTILIE

Mama Ntilie wa jirani na shule hiyo, Mwajuma Juma, alisema upo umuhimu wa kukamilisa ujenzi wa kituo cha polisi eneo hilo ili kukabiliana na matukio ya uhalifu yaliyokithiri yanayofanywa na wanafunzi na wasio wanafunzi, na kwamba ni muhimu kuharakisha ujenzi wa uzio.

Alisema wanaogopa kuwafukuza wanafunzi wanapowaona wanazurura wakati masomo kwasababu wakijaribu kufanya hivyo wanawatolea lugha chafu.

**MWALIMU SHULE JIRANI**

Mwalimu Mwamvua Miraji wa Shule ya Msingi Kilimani iliyopo Kata ya Kipunguni, alisema mtoto wake Abdull ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha tatu alivunjwa mkono shuleni na kuporwa saa na wanafunzi wenzake.

"Nilienda shule na nikamuona mwanangu amevunjwa mkono na kuporwa saa na wanafunzi wa shule ya sekondari Kelezange wakati wakiwa katika michezo iliyowakutanisha wanafunzi kutoka shule zingine," alisema.

Anaongeza kuwa alikwenda Kitunda polisi na kupatiwa PF3 kwa ajili ya kumpatia mtoto wake matibabu, na alitoa taarifa kwa Ofisa Elimu Sekondari.

Anasema Ofisa Elimu alimpa ushirikiano mpaka wanafunzi hao wawili wa Kelezange walichukukiwa hatua ya kufukuzwa shule.

"Wanafunzi hao wawili walikuwa kidato cha nne, lakini afisa elimu hakuangalia hilo, kamati zilikaa na kuamua kuwafukuza shule," alisema.

Pia, alisema wazazi wa wanafunzi wa watoto waliomvunja mkono mtoto wake wakikubaliana kumlipa saa, iliyochukuliwa na watoto wao, lakini ameambulia Sh. 20,000 kutoka kwa mzazi mmoja.

Alisema wanafunzi wa Kelezange na Misitu ni wababe hawaogopi mtu, wanavuta bangi kwa kushirikiana na watoto wa kike.

Alisema wanafunzi wa shule hizo huwavizia wanafunzi wa darasa la kwanza na kuwapora mabegi, saa, kuwavua viatu na kuvichukua.

NMB
Karibu yako

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 21 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB

**Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 21 wa mwaka wa wanahisa wa NMB utafanyika kwa njia ya mtandao saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa, Juni 4, 2021. Ajenda itakuwa kama ifuatavyo:**

21.1 MATANGAZO NA AKIDI

21.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO

21.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 20 ULIOFANYIKA TAREHE 5 JUNI 2020

21.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 20 WA WANAHISA

21.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020

21.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020

21.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI

21.8 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA KUJIUDHURU NA KUTEULIWA KWA WAKURUGENZI WA BODI

21.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOMALIZIKA 31 DESEMBA 2021

21.10 MENGINEYO

**MAELEZO MUHIMU**

1. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria Mkutano lazima atume kwa njia ya mtandao nakala yake ya risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au kitambulisho chake au kadi yake ya benki.

2. Mjumbe anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni kama zilivyorekebishwa. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni (kwa njia ya mkono au mtandao) kabla ya saa 4 asubuhi Alhamisi ya tarehe 3 Juni 2021.

3. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria kikao atahudhuria kwa njia ya mtandao. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya NMB (www.nmbbank.co.tz).

4. Wakurugenzi wamependekeza ulipwaji wa gawio la shilingi 137 kwa kila hisa, inayoleta jumla ya shilingi 68.5 bilioni kutokana na faida ya mwaka 2020.

**Tarehe za kuzingatia:**

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya tangazo:** | **14 Mei 2021** |
| **Hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **14 Mei 2021** |
| **Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **2 Juni 2021** |
| **Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:** | **3 Juni 2021 nakuendelea** |
| **Daftari la wanahisa kufungwa:** | **7 Juni 2021** |
| **Malipo ya gawio kwa wanahisa:** | **kuanzia tarehe 16 Juni 2021** |

Kwa amri ya Bodi ya Wakurugenzi,

Lilian R. Komwihangiro
Katibu wa Kampuni
7 Mei 2021

www.nmbbank.co.tz

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wahusika kuahirishwa mechi Simba, Yanga wawajibishwe

**WINGU** zito limetanda katika sakata la kuahirishwa kwa mechi ya watani wa jadi, Simba dhidi ya Yanga ikiwa ni saa tatu kabla ya mechi kuanza Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Saam.

Mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara iliyokuwa imepangwa kuchezwa saa 11:00 jioni, klabu zilitaarifiwa kusogezwa mbele kwa mchezo huo kutoka muda huo hadi saa 1:00 usiku ikiwa ni saa tatu kabla ya mechi kuanza, kwa kile kilichoelezwa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuwa ni maagizo kutoka serikalini kupitia wizara yenye dhamana na michezo.

Hatua hiyo, ilisababisha Klabu ya Yanga kugomea kucheza mchezo huo huku ikifika uwanjani muda uliopangwa awali na wachezaji kupasha misuli joto na baada ya nusu saa kumalizika ikaondoka huku Klabu ya Simba yenyewe ikiwasili uwanjani hapo baadaye kulingana muda wa pili ambao walitaarifiwa mechi hiyo itachezwa.

Kwa ujumla, si Klabu ya Yanga wala Simba inayoweza kulaumiwa katika hili, ndiyo maana hata hapakuwapo na waamuzi walioingia uwanjani kutoa uamuzi katika nyakati tofauti timu hizo zilipoingia uwanjani.

Kwa Yanga ilisimamia Kanuni ya 15 (10) ya Ligi Kuu inayohusu taratibu za michezo ambayo inataka mabadiliko yote ya michezo kujulishwa kwa pande zote husika angalau saa 24 kabla ya muda wa awali, hivyo ikawa salama.

Hivyo, pamoja na kila upande kuwa salama, huku jana TFF ikitoa tamko la kuomba radhi kwa kile kilichotokea na kuahidi kuangalia hatma ya wadau wa soka waliolipa vingilio kuingia uwanjani kushuhudia mechi hiyo, bado sisi tunaona hiyo haitoshi na wala jambo hili halipaswi kuvumiliwa lipite hivi hivi pasipo wahusika kuonekana kuwajibika ili kurudisha imani kwa mashabiki waliopoteza muda na gharama zao kubwa kwenda kushuhudia mechi hiyo.

Tunatambua wazi kuwa Yanga wangeweza kucheza mechi hiyo, lakini huenda waliona ni vema kutoa fundisho kwa wanasiasa kwani kanuni na sheria za soka lazima zizingatiwe kuliko busara na hekima ambazo zinaweza kutuchelewesha kufikia pale tunapohitaji kufika.

Hapa unaweza kuwalaumu TFF, lakini huu utaratibu wa 'maagizo kutoka juu' pasipo ufafanuzi, unalirudisha sana nyuma soka letu, na katika hilo ndio maana Shirikisho la Soka duniani (Fifa) halitaki serikali iingilie mpira na imeweka wazi sehemu ambazo serikali inaingilia mpira ni kupitia watu wa ulinzi na usalama pamoja na watu wa hali ya hewa.


Nipashe tunatambua huenda serikali ilikuwa na sababu ya msingi kabisa ya kutaka mechi hiyo isogezwe mbele muda wa kuchezwa, lakini TFF pia haiwezi kukwepa lawama kwa utaratibu iliyoutumia kwa kuziandikia barua klabu hizo kuzitaarifu hasa ikijua presha kubwa na hofu ya kuhujumiana kwa kila upande ambayo hutanda timu hizo zinapokutana.

Tunaamini serikali ilitoa sababu ya msingi kwa TFF na pengine shirikisho hilo halikuona busara kuiweka hadharani kwa umma, hivyo ilipaswa kuwaita mezani viongozi wa klabu hizo mbili na kuwaelewesha kwa kina sababu ya msingi ya kusogezwa mbele na ndipo taarifa kwa mashabiki ifuate.

Tunatambua hiyo si mara ya kwanza kwa mechi za Ligi Kuu hususan za Yanga kubadilishwa muda nje ya saa 24 na klabu hiyo kukubali kucheza, lakini kwa sababu ya presha na hofu ya hujuma watani hao wa jadi wanapokutana ndiyo maana hilo limetokea.

Hivi karibuni muda wa mechi ulibadilishwa nje ya saa 24 kinyume cha kanuni, katika mchezo wao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC na Biashara United, lakini ilikubali kucheza, lakini linapokuja suala la kukutana na mtani wake, ni tofauti, hivyo tunataka sasa kuona kanuni zikifuatwa lakini waliohusika wakichukuliwa hatua na mashabiki wakirejeshewa viingilio vyao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuna la kujifunza TFF sakata mechi Simba, Yanga

**MASHABIKI** wa soka nchini waliokwenda kuangalia mechi ya watani wa jadi kati ya Simba na Yanga Jumamosi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, walijikuta wakirudi na maumivu nyumbani.

Si ya kufungwa la hasha. Ni kwa sababu mechi hiyo haikuchezwa. Wengi waliingia uwanjani mapema tu wakitegemea kuwa ingechezwa saa 11:00 jioni.

Saa chache kabla ya mechi kuanza, ikaja taarifa ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), ikieleza kuwa imepelekwa mbele kwa saa mbili, yaani saa 1:00 usiku.

Ikasema kuwa hiyo ni baada ya kupokea maagizo kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo. Hakuna aliyedhani baada ya taarifa hiyo kitatokea kilichotokea. Ni muda mchache tu baadaye, Yanga nayo ikatoa taarifa kupingana na kile kinachoitwa kupelekwa mbele muda wa mchezo huo, ikisisitiza kuwa hiyo ni kukiuka Kanuni ya 15 (10) ya Ligi Kuu inayohusu taratibu za michezo ambayo inataka mabadiliko yote ya michezo kujulishwa kwa pande zote husika angalau saa 24 kabla ya muda wa awali.

Kila mtu baada ya hapo anajua nini kilitokea. Yanga ilipeleka timu muda wa awali na Simba ikapeleka muda uliosogezwa. Taarifa ikaja baadaye kuwa mechi imeahirishwa.

Ikawa ni maumivu makubwa. Watu wametumia nauli kutoka pande zote za nchi, wengine kutoka nje ya nchi. Tumewaona wanachama na mashabiki wa Simba tawi la Kitwe nchini Zambia nao walikuwa uwanjani. Kuna shabiki mmoja wa Yanga ametembea kwa miguu kutoka Kigoma mpaka Dar es Salaam kushuhudia mechi huyo. Wengine walikuja na usafiri wa ndege wakiwa na tiketi za kwenda na kurudi, tena zikionyesha walitakiwa waondoke saa 2:00 usiku. Ina maana mechi hata ingechezwa muda huo wa pili, wangekuwa wamechelewa ndege.

Watu wamepoteza muda, pesa, lakini kibaya zaidi baadhi walipigwa na mabomu ya machozi na Jeshi la Polisi kwa kile walichodaiwa kufanya fujo. Mashabiki hao walikuwa wakijaribu kupambana kama wanaweza kurudishiwa kiingio chao.

Lilikuwa ni doa kubwa kwa soka la Tanzania na Ligi Kuu kwa ujumla ambayo imejipambanua kuwa imepiga hatua kubwa. Kutokana na kufanya vema kwa Simba michuano ya Afrika, mashabiki wengi Afrika walikuwa wakifutilia tukio hilo kwenye televisheni, hivyo watakuwa wakishangaa kuona mechi ya 'dabi' inakuwa kama bonanza. Yanga iko sahihi kwa mujibu wa kanuni. Lakini cha kushangaza ni kwamba mashabiki wengi na wachambuzi wa masuala ya soka, wanaitupia lawama TFF moja kwa moja, hii si haki.

TFF iko chini ya serikali. Ikumbukwe kuwa kusogezwa mbele muda kwa mujibu wa taarifa hiyo ni agizo la wizara husika ambayo ndiyo serikali. Sasa tuanzie hapo.

Hata iweje, TFF isingeweza kukiuka agizo la serikali ni sawa na mfanyakazi kukiuka maagizo ya bosi wake. Halafu kama ingetokea TFF ikasema kuwa ikifanya hivyo itakiuka kanuni, mechi hiyo haingeweza kuchezwa. Uwanja ambao ingechezwa mechi ile ni wa serikali pia, hivyo ingekataza.

Ni sawa na mtu akukatalie usifanye sherehe ukapinga, ukataka kuifanya kwa nguvu, halafu kumbe utakapofanyia ni kwake. Tayari TFF imeshaomba radhi. Kuna wanaotaka waeleze ni kitu gani kimesababisha mechi isogezwe muda? Ni kwa nini wizara ilitoa maagizo hayo? Ukweli ni kwamba inaweza ikatoa au isitoe pia.

Hivi serikali ikisema kuwa ilikuwa ni kwa sababu za kiusalama kuna mtu atapinga? Halafu serikali inaweza isiseme au kufafanua ni usalama gani kwa sababu hizo hizo za kiusalama. Ni kwamba inaweza kusema, halafu hao wanaohatarisha usalama wakajifahamu kutafuta mbinu nyingine au kujificha. Hii ni dhana tu kuonyesha kuwa serikali inaweza kuahirisha mechi bila kuhojiwa.

Kuna watu wanadai kuwa serikali hairuhusiwi kujiingiza kwenye michezo, lakini niwaambie ikibidi inafanya hivyo inakuwa ni kwa nadra sana.

Ni kama ilivyofanya mwanzoni mwa mwaka jana wakati ulipoingia ugonjwa wa COVID-19 na hata iliporuhusu tena kuendelea kwa ligi.

Sitaki kusema ni sahihi au si sahihi kilichofanyika, lakini nasisitiza kuwa kuilaumu TFF kama wengi wanavyofanya si sahihi na hata wachache ambao wananyoosha kidole kwa wizara nao pia hawako sahihi.

Tatizo limeshatokea na kinachotakiwa ni ufumbuzi tu. Pia liwe ni somo, kwani siku nyingine kwenye mechi kama hizi kubwa ambazo zina mashabiki wengi, umakini mkubwa na namna ya kutoa taarifa unatakiwa.

## SATO suluhisho uhaba vyoo shuleni

**Na Maulid Mmbaga**

KAMPUNI ya Lixil watengenezaji wa vyoo vya SATO imekabidhi matundu 21 ya vyoo katika Shule ya Msingi Kerezange iliyopo Kata ya Kitunda Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam, ikiwa ni mwendelezo wa jitihada za kuisaidia serikali kutatua changamoto ya uhaba wa matundu ya vyoo kwenye shule.

Akizungumza katika hafla ya makabidhiano hayo iliyofanyika juzi shuleni hapo, Ofisa Afya wa Mkoa wa Dar es Salaam, Enezaeli Ayo, alisema adha wanayoipata wanafunzi shuleni kutokana na uhaba wa matundu ya vyoo ni moja ya vitu vinavyosababisha uzorotaji wa elimu nchini.

Alisema katika mkoa huo kuna idadi kubwa ya wanafunzi na baadhi ya shule matundu ya vyoo yaliyopo hayakidhi mahitaji kulingana na idadi ya wanafunzi na wapo katika mkakati wa kuhakikisha kuwa wanatatua adha hiyo kwenye shule, lakini tatizo linalowakabili ni uhaba wa fedha.

"Jitihada tunazozichukua kama halmashauri ya mkoa tunahakikisha kwamba hatukosi fedha kwa ajili ya kutengeneza matundu ya vyoo mashuleni, lakini kwasababu ya kuwa na vyanzo vichache vya mapato inakuwa haijitoshelezi isipokuwa tunashirikiana na wadau kama SATO katika kupuguza changamoto hii shuleni na kwenye jamii.

"Usafi wa mazingira ni mojawapo ya chachu ya maendeleo ya elimu nchini, miundombinu bora ya vyoo inasaidia afya na mahudhurio mazuri ya wanafunzi mashuleni, hivyo nawaomba wadau wengine kuendelea kuchangia uboreshaji wa mazingira ya vyoo na vifaa vya kunawia mkono shuleni ili kuisaidia jamii yetu," alisema Ayo.

Meneja wa SATO Tanzania, Justine Mbowe, alisema katika Halmashauri ya Ilala wamesaidia shule nne kuboresha vyoo kwa ushirikia na kampeni ya 'Nyumba ni Choo' na utakuwa ni mpango endelevu katika mikoa mingine nchini.

"Maono ya kutengeneza choo cha aina hii ni ili kuwafikia wananchi wote hasa wale wa hali ya chini kwa kuwapatia huduma bora ya choo kisichotoa harufu, lakini pia kinahitaji maji kidogo ambacho ni rafiki hata kwa mazingira ya vyoo vya umma," alisema Mbowe.

Pia, lengo lao ni kuboresha mazingira na ifikapo mwaka 2025 wanatarajia kusaidia watu zaidi ya milioni 100 na wanashirikiana na Wizara ya Afya nchini ili kuhakikisha kunakuwa na mazingira mazuri ya vyoo katika jamii.

Mkuu wa Shule ya Kerezange, Maria Gilaida, aliipongeza kampuni hiyo kwa kutoa kipaumbele katika suala la usafi wa mazingira huku akisisitiza kuwa mazingira bora ya shule ni suala la msingi katika maendeleo ya wanafunzi.

"Tunawashukuru SATO kwakuwa wamegusa watu wa nyanja zote kwa kutengeneza pia choo maalum kwa ajili ya walimu wenye changamoto ya ulemavu hivyo kutusaidia kwakuwa tunaweza kupokea walimu wa kila aina," alisema Gilaida.

# RC atoa wiki moja hospitali itoe huduma

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, ametoa wiki moja kwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kuhakikisha Hospital ya Wilaya ya Ilemela (Isanzu) inaanza kutoa huduma.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa ujenzi wa hospitali hiyo mwishoni mwa wiki, Mongella alisema kinachotakiwa kwa sasa ni hospitali hiyo kuanza kufanya kazi kwa sababu lengo la serikali ni kuboresha huduma za afya nchini na kwa kuwa awamu ya kwanza ya ujenzi wake imekamilika, waanze kutoa huduma.

"Nchi ambayo watu wake wana afya zenye mgogoro, ambazo siyo timamu, hata ajenda zote za maendeleo zinakuwa ngumu kutekelezwa.

"Rais wetu Samia Suluhu Hassan amejipambanua katika sekta ya afya, ni eneo ambalo linamgusa sana, hivyo huduma za afya zinaendelea kuboreshwa kwa ufadhili mkubwa na msisitizo wa serikali kuu," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, John Wanga, alisema utoaji wa huduma ya afya kwa wagonjwa wa nje umeshaanza na watatekeleza agizo la Mkuu wa Mkoa kutoa huduma za kawaida kwa mama na mtoto ambazo hazihitaji upasuaji na kushughulikia masuala ya vifaa na upatikanaji wa maji.

Alisema wananchi watarajie kupata huduma bora za afya kutoka katika hospitali hiyo ya wilaya.

Katika Hospitali ya Butimba wilayani Nyanagana, Mongella alipongeza ujenzi wa jengo la wodi za wanaume, watoto na wanawake.

Alisema jengo hilo ambalo ujenzi wake umegharimu Sh. bilioni 1.41 lilianza kujengwa mwaka 2019 na kwamba hivi sasa limekamilika na kuagiza watengeneze na chumba cha upasuaji ili kuboresha huduma.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji, Kiomoni Kimbamba, alisema vifaa vyote kwa kutolea huduma kwa mgonjwa anapolazwa vimeshanunuliwa na wanaendelea na marekebisho ili wiki hii huduma zianze kutolewa.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Dk. Phillis Nyimbi, alisema jengo hilo limejengwa kupitia mapato ya ndani ya halmashauri hiyo.



Mmoja wa wanawake wanaofanya biashara ya ndizi katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, ambaye jina lake halikufahamika mara moja, akiwa amekaa juu ya ndizi ambazo zilikuwa zinasafirishwa kwa kutumia Guta mwishoni mwa wiki jambo ambalo ni hatari kwa maisha yake. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

# Watalii waongezeka Hifadhi ya Mikumi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

IDADI ya watalii katika Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA) imeongezeka kutoka 46,908 mwaka 2012/13 hadi 60,077 mwaka 2018/19 kutokana na kukua kwa utalii wa ndani na wa kimataifa.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi na Mhifadhi Mkuu wa MINAPA, Mathew Michael, aliyasema hayo hifadhini huko mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge Ardhi, Maliasili na Utalii.

Alisema ongezeko hilo la watalii 13,169, sawa na asilimia 28.1 limechangiwa na kujitokeza kwa wingi kwa watalii wa ndani kulinganisha na takwimu za miaka minane iliyoanzia mwaka 2012/13.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka minne kulishuhudiwa ongezeko hilo akisema:

"Mwaka 2016/17, watalii wa ndani walikuwa 32,050 na watalii wa nje 27,668, mwaka 2017/18, watalii wa ndani 26,540 na watalii wa nje 24,639, mwaka 2018/19, watalii wa ndani 35,281 na wa nje 24,796 na mwaka 2019/20, watalii wa ndani 31,490 na wa nje 22,345.

Pia, alisema kumekuwa na uhusiano mzuri kati ya hifadhi na jamii kwa maana ya vijiji vinavyozunguka hifadhi kupitia shughuli za ujirani mwema ambazo ni elimu ya uhifadhi na usuluhishi wa migogoro ikiwamo ya mipaka.

Mbunge wa Viti Maalum, Asia Halamga, aliwashauri vijana nchini na vyombo vya habari kutumia fursa ya mitandao ya kijamii kutangaza na kutembelea vivutio vilivyopo vya utalii badala ya kutumia muda wao wingi kwa masuala ambayo hayana faida kwa taifa.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Aloyce Kwezi, aligiza Wizara ya Maliasili na Utalii kuboresha miundombinu ya mawasiliano katika hifadhi zote za Mkoa wa Morogoro ili kuongeza vivutio kwa watalii wa ndani na nje na hivyo kuongeza mapato.

"Suala la mawasiliano kwenye hifadhi za taifa ni lazima ziboreshwe ili kuhamasisha zaidi kutangaza utalii kwani kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wadau wa utalii kuwapo kwa tatizo la mawasiliano wanapokuwa hifadhini," alisema.

# Ndalichako azindua tovuti elimu mtandao

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Vodacom Tanzania imezindua tovuti ya E-Fahamu, ambayo ina lengo la kuwasaidia wanafunzi na walimu kupata vitabu vya kiada na ziada kwa njia ya kidijitali bila malipo.

Vilevile kampuni hiyo imeshirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kuweka vitabu na mitaala iliyopitishwa na TET kwenye mfumo huo, nakala zaidi ya 80 za machapisho ya kiada, nakala zaidi ya 1,020 za machapisho ya ziada na katuni 18 zenye masomo zikiwekwa.

Akizindua mfumo huo mwishoni mwa wiki, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, aliishukuru Vodacom kwa kuja na ubunifu huo uliolenga kuboresha hamasa ya wanafunzi kujisomea.

"Kama tunavyojua watoto wetu wanapenda kuchezea simu, sasa badala ya kuangalia mambo yasiyofaa, Vodacom Tanzania imewapa fursa ya kupata maudhui ya masomo na kubwa ni kuwa maudhui haya yatapatikana bure hivyo watoto wa hali zote za kiuchumi watanufaika, nawapongeza sana kwa hili," alisifu.

Profesa Ndalichako pia alipongeza juhudi zinazofanywa Vodacom Tanzania Foundation kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) zinazowafikia wanafunzi wengi hususani wa vijijini.

Alizitaja huduma hizo kuwa ni pamoja na kompyuta na vipanga njia (routers) kwa shule za sekondari nchini.

Mpaka sasa kompyuta 48, vipanga njia 24 pamoja na SimCard zimetolewa kwa shule za sekondari 24 Katika awamu ya kwanza wakati awamu ya pili wamepanga kuzifikia shule za sekondari 163 na kwamba tayari shule 151 zimefikiwa kwenye mikoa mbalimbali nchini na kutoa kumpyuta 556, printer 83 na vipanga njia 151 kwa lengo la kuwanufaisha wanafunzi na waalimu 4,000.

"Tunawashukuru sana kuleta tabasamu kwa wanafunzi wetu, hususan waliopo maeneo ya vijijini," Waziri Ndalichako alisifu.

Alisema ni imani yake kuwa kupitia jukwaa la E-Fahamu, ufaulu utaongezeka kwa sababu walimu na wanafunzi watakuwa na uwezo wa kupata maudhui mbalimbali, hivyo kujiongezea maarifa yatakayowawezesha wanafunzi kufaulu mitihani yao katika ngazi mbalimbali.

"Ninawaomba Vodacom Tanzania Foundation muendelee kuongeza idadi ya vitabu katika jukwaa hili ili kuongeza wigo kwa walimu na wanafunzi kupata maudhui mengi zaidi, na hivyo kusaidia katika kujifunza masomo mbalimbali," alishauri.

Profesa Ndalichako alitumia fursa hiyo kutoa rai kwa kampuni zingine kuiga mfano wa Vodacom Tanzania, kupitia taasisi yake ya uwajibikaji kwa jamii ili kuhakikisha wanaiunga mkono serikali katika ajenda yake ya kuhakikisha wanafunzi wanakuwa na mazingira mazuri ya kupata elimu bila gharama yoyote.

Awali, Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation - Rosalynn Mworia, alisema mfumo huo ambao zamani ulijulikana kama Instant Schools, umeongeza maudhui kutoka TET ili kupata matokeo chanya zaidi kwa wanaosoma kwa mfumo wa Kiswahili na Kiingereza.

"Kupitia jukwaa hili, mtu yeyote anaweza kutafuta, kupakua na kupata maudhui mbalimbali ikiwamo yale ya elimu ya darasani na stadi za kazi kupitia mtandao wa Vodacom kwa kutembelea tovuti hii.

# TAKUKURU yajitosa migogoro ya ardhi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Morogoro, imeanza kufuatilia migogoro ya ardhi iliyoanza kuibuka tena katika baadhi ya maeneo, ili kubaini mianya ya rushwa na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika wote kwa mujibu wa sheria.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Morogoro, Janeth Machulya, alitangaza hatua hiyo mwishoni mwa wiki alipotoa taarifa kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu kazi zilizotekelezwa katika mkoa huo kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu.

Alisema mbali na ufuatiliaji huo, katika kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka huu, taasisi hiyo pia imejiwekea mikakati kadha ikiwamo kuchunguza taarifa za ubadhirifu zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika baadhi ya taasisi za umma ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Machulya alisema kuwa katika kipindi hicho, TAKUKURU Mkoa wa Morogoro iliendelea kushughulikia tuhuma za vitendo vya rushwa na kufanikiwa kuwafikisha mahakamani watuhumiwa wapatao 12 ambao wamefunguliwa jumla ya kesi 10.

Mbali na kuendelea kushughulikia tuhuma hizo, alitoa angalizo kwa watendaji wasio waaminifu katika mamlaka zinazohusika na ardhi, hasa halmashauri, kutekeleza majukumu kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

"Watendaji hawa wanapaswa kujua wanayo dhamana kubwa ya kuwahudumia wananchi na kuwatatulia kero zao bila kujihusisha na vitendo vya rushwa," alikumbusha.


Katika kudhibiti vitendo vya rushwa, kiongozi huyo alisema TAKUKURU Mkoa wa Morogoro imefanikiwa kuokoa Sh. milioni 114.448 ambazo zilikuwa mikononi mwa viongozi wa Vyama vya Ushirika na SACCOS kwa nia ya kujinufaisha kinyume cha sheria.

Alibainisha kuwa kwa kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu, TAKUKURU Mkoa wa Morogoro pia ilifuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayoendelea mkoani humo yenye thamani ya Sh. bilioni 3.7.

Machulya alisema TAKUKURU ilibaini kuwapo kwa ukiukwaji wa masharti katika mikataba ya baadhi ya miradi na imezishauri halmashauri husika kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati na inafikia thamani tarajiwa.

Alisema kuwa kwa kipindi hicho cha miezi mitatu, taasisi hiyo ilianzisha utaratibu wa 'TAKUKURU INAYOTEMBEA' kwa kutenga siku moja kila mwezi kwa ajili ya kusikiliza kero za rushwa kwa kuwafuata wananchi huko waliko na kuzitafutia ufumbuzi.

Machulya alitoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na taasisi hiyo kutokomeza vitendo vya rushwa mkoani Morogoro.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (kushoto), akipokea mfano wa hundi ya thamani ya Sh. milioni 15 kutoka kwa Mhazini Mkuu wa Benki ya NMB, Azizi Chacha, kwa ajili ya udhamini wa mashindano ya kitaifa ya Sayansi na Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) yaliyoanza jana uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma ,wengine katika picha kutoka kushoto ni Naibu Waziri Elimu,Omari Kipanga na watatu ni Katibu Mkuu wa wizara hiyo Dk. Leonard Akwilapo

# Mtaka ataka uwezo wa watendaji zabuni za umma

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, amezitaka taasisi za Serikali mkoani humo kuhakikisha zinawajengea uwezo wafanyakazi wake kuhusu sheria na taratibu za kufanya ununuzi wa umma ili wawe na ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

Aliyasema hayo wakati wa hafla ya kufungua mafunzo ya sheria ya ununuzi wa umma na Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS), yanayotolewa na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), yaliyofanyika mkoani humo katika Mji wa Bariadi, mwishoni mwa wiki. Takribani washiriki 92 walihudhuria, ambao ni Wajumbe wa Bodi za Zabuni, Wakuu wa Idara Tumizi (user departments), watumishi kutoka vitengo vya Ununuzi wa Umma (PMU), wanasheria, na wakaguzi wa ndani kutoka Halmashauri zote za Mkoa wa Simiyu na taasisi mbalimbali za mkoa huo.

Mtaka aliyekuwa mgeni rasmi, alisema taasisi za umma zimekuwa na chagamoto nyingi kuhusu michakato ya ununuzi wa umma. Alisema sababu kubwa ni watendaji wanaojihusisha na shughuli za ununuzi wa umma kutokuwa na uelewa wa kutosha wa sheria na taratibu za kufanya michakato hiyo.

"Ni muhimu sana kushiriki mafunzo wakati uko kazini kuhusu kazi unayoifanya. Changamoto ni kwamba baadhi ya wafanyakazi wa Serikali, akishawasilisha cheti chake na bahati nzuri akapata kazi, basi hahudhurii tena mafunzo yoyote wakati yuko kazini. Hii inasababisha matatizo mengi katika utekelezaji wa miradi, kwakuwa msimamizi au mtendaji wa taasisi ya umma anakuwa hafahamu mambo muhimu," alisema Mtaka.

Alitoa wito kwa watumishi wa mkoa huo kuhakikisha wanaitumia ipasavyo fursa ya mafunzo hayo yanayotolewa na PPRA, ili kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana kwenye miradi inayofanyika mkoani humo yenye lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.

Aidha, alizielekeza taasisi za umma za mkoa huo kuhakikisha zinawagharamia na kuwaruhusu watendaji wanaostahili kuhudhuria katika Kongamano la Mwaka la Ununuzi wa Umma, litakalofanyika jijini Dodoma kuanzia Mei 6-27, mwaka huu na jijini Arusha kuanzia Juni 1-3, mwaka huu kwa kuwa ni fursa ya kipekee ya kuwakutanisha wadau mbalimbali wa ununuzi wa umma ili kujadili, kubadilishana uzoefu, kujifunza na kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili.

HABARI KITAIFA

# W'biashara wagoma kulipa ushuru wa halmashauri

Na Hamisi Nasri, MASASI

KATIBU Tawala Mkoa wa Tabora ametakiwa kupeleka Wataalamu wa ukaguzi kutoka maeneo mbalimbali kwenda kufanya ukaguzi kwenye mradi wa ujenzi wa nyumba ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora ili kujiridhisha kama fedha zilizoshatumika zinalingana na kazi zilizofanyika.

Hatua inayofuatia nyumba hiyo kujengwa kwa zaidi ya miaka 10 na kugharimu fedha nyingi wakati Jaji Mfawidhi akiendelea kuishi katika nyumba ya kupanga.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora , Dk. Philemon Sengati (pichani), alipotembelea kuona hatua ilipofikia nyumba ya kiongozi huyo, baada ya uongozi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora kumwomba kuwasaidia kusukuma mbele suala hilo.

Alisema hadi hivi sasa nyumba hiyo imegharimu Sh. milioni 405, lakini bado kazi nyingine kama kuunganisha maji, kujenga kibanda cha walinzi na kukamilisha uzio hazijakamilika.

Dk. Sengati alisema licha ya Serikali kuvunja mkataba na kampuni ya ukandarasi ya Nice Standard Investment Ltd ya Dar es Salaam mwaka 2014 kwa sababu ya kazi kwenda polepole na kukabidhi kwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) bado kazi inaendelea kusuasua.

Alisema kitendo cha kuendelea kuichelewesha kumesababisha baadhi ya maeneo kuanza kuchakaa na kitaiongezea serikali gharama mpya na kuwataka TBA kuwa wazalendo wanapopewa kazi

Naye Mtendaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Cosmas Lugora, alisema mahakama imekuwa ikitumia fedha nyingi kulipia pango la nyumba ya Jaji Mfawidhi kila mwezi wanalipa Sh. milioni moja.

Alisema tangu mwaka 2010 ambapo nyumba ndipo ilipotakiwa kukamilika, wametumia fedha nyingi ambazo zingesaidia kuboresha huduma nyingine za utoaji wa haki kwa wananchi.

Lugora alisema kila mwaka wamekuwa wakiwasiliana na TBA na kupewa ahadi ambazo hawazitimizi na kumuomba Mkuu wa Mkoa awasaidie kuuhimiza wakala huo kumalizia nyumba hiyo ili Jaji Mfawaidhi aweze kupata sehemu nzuri ya kuishi na kutekeleza majukumu yake vema.

Kaimu Meneja wa TBA Mkoa wa Tabora, Abraham Ndazi, alisema ujenzi ulisimama tangu Novemba 2017, kutokana na ukosefu wa fedha za kumalizia kazi zilizobaki.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, akikagua bidhaa mbalimbali zilizozalishwa na wajasiriamali wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam katika fainali za Ubunifu na Ujasiriamali Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Siku ya Wanafunzi ya Ubunifu na Ujasiriamali inayoadhimishwa Mei 08, kila mwaka, " katika ukumbi wa Nkrumah, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serengeti wapata mradi wa maji wa mil. 220/-

Na Mwandishi Wetu

WAKAZI wa Wilaya ya Serengeti mkoani Mara wamepata ukombozi wa maji, baada ya kuzinduliwa mradi wenye thamani ya Sh. milioni 220.

Mradi huo ulizinduliwa jana na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) katika Kijiji cha Machochwe zikiwa ni jitihada zake za kusaidia upatikanaji wa huduma ya maji salama kwa wananchi wa eneo hilo.

Mradi huo wenye uwezo wa kuhudumia watu 12,000, unahusisha uchimbaji wa kisima,ununuzi wa tanki la maji na pampu yenye uwezo wa kuvuta lita 7,500 kwa saa

Akizungumza wakati wa kukabidi kisima hicho, Mkurugenzi wa Uhusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha alisema kampuni hiyo kupitia mradi wa 'Maji ni Uhai' imesaidia uchimbaji wa visima vilivyosaidia upatikanaji wa majisafi na salama katika maeneo mbalimbali ikiwamo Iringa, Kilimanjaro, Mwanza, Tanga, Ruvuma, Dar es Salaam, Pwani na Dodoma ikiwezesha upatikanaji wa huduma hiyo muhimu kwa zaidi ya watu milioni moja.

Wanyancha alisema mradi wa Machochwe hautasaidia tu kuboresha afya za wakazi wa eneo hilo, bali pia utaongeza uzalishaji mali kwa kuwa wasichana na akina mama hawatatembea tena umbali mrefu kutafuta maji na kuongeza kuwa utawapa wasichana muda zaidi wa kuhudhuria shule.

"SBL inayo sera inayolenga kuboresha maisha ya jamii zetu na Maji ni Uhai ni moja kati ya vipaumbele ambavyo vimeelezewa kwenye malengo ya kampuni yetu kuboresha maisha ya jamii inayotuzunguka," alisema Wanyancha. Mkurugenzi huyo alitaja vipaumbele vingine ni kutoa ujuzi kwa ajili ya maisha, Utunzaji wa Mazingira na Unywaji wa Kiasi.

Zaidi, Wanyancha alisema SBL inao mpango wa kusaidia wakulima ambao kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita umefanikiwa kuwafikia na kuwasaidia wakulima 400 kwa kuwapatia msaada wa kitaalamu na kifedha hivyo kuweza kuboresha maisha yao na ya jamii zao

"Kupitia mpango huu, SBL imeweza kupata malighafi kwa ajili ya uzalishaji wake kutoka tani 0 hadi 17,000 zinazozalishwa na wakulima wa ndani jambo ambalo limesaidia ukuwaji wa kampuni na kuongeza kipato kwa wakulima pia," alisema.

Mgeni rasmi katika uzinduzi wa mradi huo Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, Nurdin Babu, alishukuru SBL kwa kutoa msaada huo uliokuwa ukihitajika sana na kuongeza kuwa kampuni hiyo imekuwa mdau mkubwa wa maendeleo hapa nchini.

# Deni Dola 68,000 laficha tumbaku

Na Shaban Njia, KAHAMA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, limeibuka na hoja ya wakulima wa zao la tumbaku kuficha tumbaku kutokana na kutolipwa madai yao ya mauzo katika msimu uliopita kiasi cha Dola 68,000 za kimarekani na kusababisha Halmashauri hiyo kukosa mapatoa.

Wakulima hao ni kutoka katika vyama vya msingi vinne vya Maliza Amcos LTD Dola 14,000, Ibambala Amcos Ltd Dola 27,526.88, Kasandalala Dola 26,615 na Amcos ya Isajangudu Dola 208.62 vikiwa vinadai fedha hizo kutoka katika kampuni za ununuzi wa zao ya Grad Tobacco na Jaspani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira, Kulwa Shoto, aliyabainisha hayo wakati kikao cha madiwani cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2020/2021 kuanzia Januari hadi Machi, alisema mpaka sasa wakulima wanaingia msimu mpya wa masoko hawajalipwa fedha wanazodai kampuni.

Alisema wakulima wameanza kuficha na kutopeleka tumbaku sokoni kwa madai mpaka watakapolipwa fedha wanazozidai na itasababisha Halmashauri kuendelea kukosa mapato yake kupitia zao hilo na kwamba licha ya kudai fedha hizo, nao wanadaiwa na taasisi za kifedha kiasi cha zaidi ya Sh. milioni 511.

Mwenyekiti huyo ambae ni Diwani wa Kata ya Bukomela alisema, kilimo hicho kinaendeshwa kwa mikataba kati ya wakulima na wanunuzi wa zao hilo na walipaswa kulipwa fedha zao ndani ya siku 14 baada ya kuuza tumbaku, lakini cha kushangaza takribani mwaka mzima hajawalipwa na masoko mapya yamefunguliwa.

Nae Diwani wa Bulungwa, Kazwani Mteganoni, alisema wakulima wanashindwa kupekea tumbaku sokoni kwa kuwa wanadai na wanalazimishwa kwa nguvu kufunga mikataba upya na kampuni wanazozidai ili wawauzie tumbaku ya msimu huu.

Naye Diwani wa Nyamilangano, Robert Mihayo, alisema, Halmashauri hiyo inategemea mapato yake kwa asilimia kubwa kutoka kwenye zao la tumbaku na kama wahusika wasipolichukua suala hilo kwa mapana zaidi, litasababisha Halmashauri kukosa mapato katika mauzo ya masoko msimu huu.

Akijibu malalamiko hayo kwa niaba ya Mkurugenzi, Ofisa Kilimo wa Halmashauri hiyo, Anna Ng'ongi, alisema awali wakulima walikuwa wanadai Dola 80,000 kimelipwa mpaka Dola 68,350 na suala hilo linashughulikiwa na bodi ya tumbaku kwa kushirikina na Wizara ya Kilimo.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU), Emmanuel Charahani, alisema sio halmashauri hiyo pekee inadai fedha hizo, bali wilaya nzima ya Kahama wakulima wanadai kiasi cha Dola 40,000 na wadaiwa wameitwa na Waziri wa Kilimo kuangalia namna ya kulipa madeni hayo.

# Waziri ataka uhamasishaji kulima mazao ya mafuta

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geofrey Mwambe, amesema ipo haja ya kujenga uwezo ma kuhamasisha wakulima kulima mazao yanayozalisha mafuta, ikiwamo mchikichi, kwa ajili ya mahitaji ya ndani na nje ya nchi.

Amesema serikali inatambua kuna upungufu wa mafuta ya kula, kutokana na uwezo wa nchi kuwa mdogo katika uzalishaji na kwamba mahitaji ni tani 564,000 kwa mwaka huku uwezo ni 206,000.

Mwambe aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, mkoani Tabora, wakati akizindua kitabu cha mwongozo wa uwekezaji mkoani humo.

Alisema ipo mikoa ikiwamo Tabora ambayo ina uwezo wa kuzalisha mazao au mbegu za mafuta ikiwamo, pamba, michikichi na kwamba fursa hiyo ikitumika vizuri itainua kiwango cha uchumi wa wananchi na taifa.

"Mafuta ya kula ni muhimu, sasa tujenge uwezo wetu kuhamasisha wakulima kulima mazao yanayotoa mbegu ambazo huzalisha mafuta. Tabora mnazalisha pamba kwa wingi, mchikichi pia, maendeleo ya nchi ni mchakato unaohitaji kuwekeza," alisema Mwambe na kuongeza:

"Mafuta ni bidhaa muhimu sana, tunakula yanaingia mwilini, ni lazima kujihakikishia usalama wake. Ni ngumu kupika chakula bila mafuta, tunaagiza mafuta ya mawese, yatokanayo na mchikichi kutoka Singapore, Malaysia, Indonesia."

Mwambe, alisema uwekezaji ni kuwekeza rasilimali kidogo kidogo ili kukusaidia mahitaji ya baadae akisema mkakati wa wizara ni kuzalisha malighafi ambazo hutoa bidhaa tofauti, badala ya kuagiza nje ya nchi.

Alisema wawekezaji wa mafuta nchini wapo wa kutosha isipokuwa upatikanaji wa malighafi mdogo.

Kadhalika, Mwambe aliwahamasisha viongozi wa mkoa huo, uwezo wa uwekezaji kiuchumi kwa wakazi wa mkoa huo ili wafikie uchumi wa kati.

"Tabora kwa mwaka ina kipato cha Sh. trilioni tano, ina maana kila Mwanatabora hupata Sh.milioni mbili hadi tatu kwa mwaka. Tafsiri yake hamjafikia uchumi wa kati ikilinganishwa na kiwango cha kitaifa.

"Mwaka jana tuliingia katika uchumi wa kati, vigezo vya Benki ya Duia ni dola 1,036 ili kuingia katika uchumi huo, baada ya kupiga hesabu, WB ilibaini tumevuka hadi 1,080, tumevuka. Ila Mkoa wa Tabora mpo katika dola 800 hivyo hamjafikia kiwango hiki."

Mwambe alisema kila mkoa ukijitathmini na kijikita katika kilimo cha mazao tofauti ikiwamo matunda itasaidia kukuza uchumi.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Philemon Sengati, alisema asilimia 90 ya ardhi iliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji haijapimwa, ili kuvutia wawekezaji kuwekeza.

Alisema serikali ilipovibinafsisha viwanda vitatu vya mkoa huo, ikiwamo cha nguo, bado havijasaidia kuongeza tija husan ajira na uzalishaji na kwamba yaliyomo kwenye mwongozo huo yatasidia kukuza uchumi wa mkoa huo.



Wawakilishi wa Bodi ya Wakurugenzi na menejimenti ya kampuni ya Assemble Insurance na wadau wa jijii la Mwanza wakati wa hafla ya Iftar iliyoandaliwa na kampuni hiyo kwa wadau. **MPIGAPICHA WETU**

## Madiwani wakosoa mpango kukopesha pembejeo wakulima

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

SERIKALI imeshauriwa kusitisha mpango wake wa kuwakopesha pembejeo za kilimo wakulima wa korosho kwa msimu wa 2021/2022 hadi pale itakapofanya tathimi yakinifu na kujiridhisha kuhusu ufanisi na takwimu sahihi za wakulima wanaostahili kupatiwa.

Ushauri huo ulitolewa jana wilayani Masasi mkoani Mtwara na Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi katika kikao cha kujadili na kupitisha hoja mbalimbali za halmashauri.

Madiwani hao walisema kuna uwezekano mkubwa kwa ugawaji wa pembejeo za kilimo bure kwa wakulima ukasababisha malalamiko mengi kwa wakulima kwa kuwa wapo baadhi ya wakulima ambao watakosa pembejeo hizo.

Diwani wa Mpindimbi (CCM), Samson Bushiri, alisema serikali imeazimia kutoa pembejeo za korosho kwa wakulima bure kwa sasa na mkulima atalazimika kukatwa Sh.110 baada ya kuuza korosho zake ghalani, na kiukweli wakulima wengi hawana fedha kwa sasa za kununua pembejeo dukani. Bushiri alisema licha ya mpango huo mzuri wa serikali madiwani wanaona kuwepo kwa changamoto ya pembejeo hizo kutoletwa kwa wakati kwani hadi sasa bado pembejeo hizo hazijatolewa kwa wakulima wakati muda wa kupulizia umeshafika kwa baadhi ya maeneo.

Alisema changamoto ya pili ni kama pembejeo zina ubora unaotakiwa kwa wakulima, kwa sababu kila mkulima huwa ananunua pembejeo ambayo anaona inamfaa kulingana na maeneo anayolima mikorosho yake, hivyo serikali inatambuaje hilo.

Alisema serikali imetoa muongozo huo wa kila mkulima kukatwa Sh.110 kwa ajili ya marejesho ya pembejeo za kilimo, lakini wapo wakulima ambao hawatambuliwi na serikali na wanauza korosho zao ghalani na watakatwa kiwango hicho cha fedha wakati wao hawatapewa pembejeo kwa sababu hawapo kwenye takwimu ya serikali ya watakaopata salfa hizo, lakini inaonyesha watakatwa fedha hiyo.

Naye Diwani Chikorpola, Edward Mahelela, alisema kuna shida kubwa ya maelekezo ya serikali juu ya mpango wake wa kutoa pembejeo za kilimo kwa wakulima, ambapo maelekezo hayo yanasema kila mkulima anayepeleka mazao yake kuuza ghalani atakatwa Sh.110 kwa lengo la kurejesha ghalama za pembejeo bila kuangalia mkulima aliyekopeshwa pembejeo hizo na serikali.

"Kwa utaratibu huu inamaana kuwa wapo wakulima ambao watakatwa fedha nyingi wakati pembejeo walizochukua ni kidogo na wapo watakaokatwa fedha kidogo wakati pembejeo walizokopeshwa ni nyingi ... kwa sasa serikali wamechelewa kuanza utekelezaji wake, hivyo ni bora wangesitisha msimu huu na wakaanza msimu ujao kama majaribio," alisema Mahelea.

Naye mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Ibrahimu Chiputula, alisema wanaishauri serikali kuangalia upya mpango huo kwani kabla haujaanza utekelezaji wake unaonyesha changamoto kadhaa ambazo zitawafanya wakulima kupunjwa fedha zao

## Assemble yaahidi huduma bora bima

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Bodi ya Bima ya Assemble, Dk. Edmund Mndolwa, aliwahakikishia wadau kwamba kampuni hiyo itaendelea kutoa huduma bora na za kipekee ambazo zitakidhi na kuzidi mahitaji ya wateja na wadau wake.

Alitoa ahadi hiyo mwishoni mwa wiki jijini Mwanza Kampuni ya bima ya Assemble ilipoandaa hafla ya Iftari kwa wadau ikiwa na lengo la kulitambulisha rasmi jina jipya la Assemble Insurance Company Limited (iliyokua ikijulikana kama AAR Insurance) kwa wadau wake wa Mwanza pamoja na kuwashukuru wateja na wadau wote ambao wamekuwa wakiunga mkono kampuni hiyo mpaka sasa.

Alisema: "Ni ahadi yetu kuwa kampuni ya Assemble Insurance itaunga mkono na kuonyesha jitihada katika kuufikia umma kwenye kutoa huduma afya kwa asilimia 100. huku ikiendelea kutoa huduma bora za bima kwa kufuata sheria za nchi".


"Napenda niwahakikishie kuwa, kwa kujiunga na kuwa sehemu ya wanufaika wa Assemble Insurance Company Limited, mko kwenye mikono salama na tutahakikisha kuwa mnapata huduma bora zaidi za bima, kwa njia rahisi na kwa haraka," alihitimisha Dk. Mndolwa.

Hafla hii muhimu inafanyika baada ya hafla kubwa ya uzinduzi rasmi wa jina jipya la Assemble Insurance uliofanyika Mkoani Dar es Salaam,Aprili 30, 2021. Tukio hili lilikuwa kilele cha juhudi kubwa za pamoja zilizoanza miaka 35 iliyopita, wakati Kampuni ya Bima ya AAR ilipoanza shughuli zake katika Kanda ya Afrika Mashariki Mkurugenzi Mtendaji wa Bima ya Assemble, Violet Mordichai, alisema Taasisi binafsi na za Serikali, wateja, watoa huduma, wadau na watu binafsi wamechangia kwa njia moja au nyingine kuifanya kampuni hii kueneza mizizi yake Tanzania.

"Ningependa kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zetu za dhati kwa wateja wetu wote wa Arusha, taasisi binafsi na za serikali na wadau wote kwa kuonyesha kutuamini na kutuunga mkono mpaka hapa tulipo. Hii ni hatua kubwa na ya kihistoria kwa kampuni, na tusingeweza fanikisha hatua hii bila ya nyinyi," alisema.

Aliendelea kusisitiza kuwa Kampuni ya Bima ya AAR ilikua ikijikita zaidi katika utoaji wa huduma ya bima ya afya, Lakini sasa kupitia Kampuni ya Bima ya Assemble itajikita katika utoaji wa huduma za bima za afya na zisizo za afya. Na hii ni moja kati ya sababu za kuchagua jina 'Assemble', ambalo kwa kiswahili lina maana ya 'mkusanyiko'. Jina hili linaakisi mkusanyiko wa aina mbalimbali za huduma za bima zitakazokuwa zikitolewa chini ya mwamvuli mmoja.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 WALIOITENDEA HAKI JEZI NAMBA 10 DIMBANI UK. 12




# NYOTA WA5 WANAOMALIZA MIKATABA YAO MWEZI HUU

**MADRID, Hispania**

KATIKA miezi inayokuja, baadhi ya wachezaji wakubwa duniani wanakuwa huru baada ya kumalizika kwa mikataba yao na klabu zao, huku wakiwa wameshindwa kufikia makubaliano na timu zao.

Soka la Ulaya kwa msimu wa 2020-21, linaelekea mwisho na klabu zikijipanga kutafuta wachezaji wapya ili kuimarisha vikosi vyao.

Makala haya yanawachambua wachezaji watano ambao mikataba yao inafikia mwishoni Mei hii.

**#5. Gini Wijnaldum | Liverpool**

Gini Wijnaldum amekuwa mchezaji nguzo wa Liverpool kwa miaka mingi na mmoja wa wachezaji anayeaminika zaidi na kocha Jurgen Klopp klabuni hapo. Hata hivyo, bado hajafikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na anaonekana kama yupo njiani kuondoka hapo kwenye dimba la Anfield. Raia huyo wa Uholanzi alikuwa akihusishwa na Barcelona kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini dili hilo likafeli dakika mwisho.

Kipindi hiki cha majira ya joto inaonekana kama Wijnaldum anaondoka na kwenda kwa miamba hao wa LaLiga akiwa mchezaji huru. Liverpool walimpa ofa ya mkataba mpya, lakini inaonekana hana mpango nao.

Wijnaldum pia anawaniwa na Inter Milan na Paris Saint-Germain.

**#4. Giorgio Chiellini | Juventus**

Anachukuliwa kama mmoja wa walinzi bora wa wakati wote, Giorgio Chiellini inaonekana kwamba anaachana na Juventus kipindi hiki cha majira ya joto. Beki huyo wa kimataifa wa Italia amekuwa na klabu hiyo tangu mwaka 2005.

Hata hivyo, katika umri wake wa miaka 36, ni wazi kwamba ubora wake umefikia mwisho na kuna uwezekano akastaafu soka mwishoni mwa msimu huu.

Amecheza mechi 500 katika mashindano yote kwa Juventus na ameshinda mataji 14, yakiwamo tisa ya Ligi Kuu Italia, Serie A.

**#3. Memphis Depay | Lyon**

Memphis Depay amerudi kwenye ubora wake baada ya kuwa na wakati mgumu kule Old Trafford na anatarajia kutafuta maisha mengine kipindi hiki cha majira ya joto. Kama ilivyo kwa Wijnaldum, yeye pia anahusishwa na mpango wa kwenda Barcelona.

Miamba hao wa Catalunya wana nafasi kubwa ya kumsajili kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anaripotiwa tayari amefikia makubaliano binafsi ya kutua pale Camp Nou.

Depay pia anawaniwa na miamba wa Ligi Kuu England, Liverpool ambao wamemtaka kwa miaka kadhaa.

**#2. Sergio Ramos | Real Madrid**

Nahodha wa Real Madrid, Sergio Ramos, bado hajafikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na klabu yake. Mlinzi huyo wa Uholanzi ni mmoja wa wachezaji bora zaidi kwenye historia ya klabu hiyo, na 'Los Blancos' hao bado hawajafikia kile anachokitaka.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 35, ndio yupo kwenye kipindi chake cha jioni cha kucheza soka, lakini klabu kadhaa zimeonyesha nia ya kutaka huduma yake. Hata hivyo, Rais wa Real Madrid, Florentino Perez, amedokeza kwamba anataka kumbakisha klabuni hapo, lakini kwa masharti ya kukubali kupunguziwa mshahara.

Majaliwa ya Ramos bado hayajajulikana na ripoti zinaonyesha kuwa anaweza kutimkia kwenye Ligi Kuu England ambako Manchester United wameonyesha nia ya kumtaka.

**#1. Lionel Messi | Barcelona**

Jina la Lionel Messi limetawala vyombo vya habari kwa kutofikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na Barcelona.

Nahodha huyu wa Barcelona, mkataba wake unafikia ukingoni kipindi hiki cha majira ya joto. Miamba hao wa Catalunya wanahaha kuhakikisha wanafikia mahitaji ya mchezaji huyo.

Gwiji huyo wa Argentina kipindi cha majira ya joto kilichopita aliomba kuondoka klabuni hapo, kabla ya kubadili uamuzi. Mambo mengi yamebadilika pale Barcelona, huku Rais Josep Bartomeu akiondoka na nafasi kuchukuliwa na Joan Laporta.

Messi kwa sasa anaonekana kama mtu mwenye furaha kubwa na kuna uwezekano akaongeza mkataba wa kubaki hapo Camp Nou.

## ISIKUPITE

146- Ni nafasi alizotengeneza Mesut Ozil katika msimu wa 2015-16, ambazo bado ni nyingi zaidi kuwahi kutengenezwa na mchezaji kwa msimu mmoja tangu Opta ilipoanza kukusanya takwimu hizo mwaka 1996.






# WACHEZAJI 10 WALIOITENDEA HAKI JEZI NAMBA 10 DIMBANI

**LONDON, England**

BILA shaka jezi namba 10 ni maarufu zaidi kwenye mpira wa miguu duniani na ina umuhimu mkubwa. Kiutamaduni, inavaliwa na kiungo mshambuliaji na ina alama za neema, ubunifu na mabao.

Baadhi ya wachezaji wakubwa wamekuwa wakivaa jezi namba 10. Soka la kisasa linaonekana kutokuwa na viungo wengi washambuliaji, nyota kama Mesut Ozil na James Rodriguez ndio wameonekana kuibeba jezi namba 10 kwa viungo wa hivi karibuni.

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10 ambao wameifanyia makubwa jezi namba 10, hawa hapa...

**#10. Francesco Totti**

Mchezaji wa klabu moja, Francesco Totti, alikuwa kijana wa dhahabu wa Roma na anachukuliwa ndiye gwiji mkubwa wa klabu hiyo.

Totti alianza kuichezea Roma mwaka 1992, lakini alianza kuonekana wa muhimu msimu wa 1994/95. Akiwa na uwezo wa kucheza nafasi yoyote ya ushambuliaji na akatamba kwa miongo miwili.

Yeye ndiye mfungaji wa pili wa wakati wote kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A.

Nyota huyo wa zamani wa Italia, pia ndiye mchezaji aliyecheza mechi nyingi zaidi na kufunga mabao mengi zaidi kwa Roma. Totti amecheza jumla ya mechi 785 katika mashindano yote kwa Roma, akifunga mabao 307 na kutoa pasi za mwisho 184. Ameshinda taji la Serie A mara moja na alikuwa sehemu ya kikosi cha Italia kilichotwaa Kombe la Dunia mwaka 2006, kabla ya kustaafu soka mwaka 2017.

**#9. Wayne Rooney**

Wayne Rooney alikuwa mfungaji mzuri wa mabao tangu akiwa kijana mdogo.

Ni zao la kutoka akademi ya Everton na alifunga bao la ushindi dhidi ya Arsenal akiwa na umri wa miaka 16. Kipaji chake kikaifanya Manchester United kulipa pauni milioni 33 mwaka 2004 na kumsajili Rooney akiwa na umri wa miaka 18, uhamisho ambao baadaye ulizaa matunda.

Mchezaji huyo wa zamani wa England, alitumia misimu 13 pale Old Trafford na kuwa mfungaji wa muda wote wa klabu hiyo na mfungaji namba mbili wa wakati wote wa Ligi Kuu England.

Rooney mwenye umri wa miaka 35 sasa, aliondoka Manchester United mwaka 2017. Baada ya kutamba Everton na DC United, Rooney kwa sasa ni kocha wa Derby County.

**#8. Roberto Baggio**

Wengi wanamchukulia Roberto Baggio kama mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote wa Italia.

Baggio amezichezea klabu kadhaa za Italia, huku akianza kutengeneza jina akiwa Fiorentina. Baadaye akajiunga na Juventus mwaka 1990 kwa pauni milioni 11.5.

Alicheza mechi 200 kwenye mashindano yote akiwa na 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin akifunga mabao 115. Baggio alifurahia pia mafanikio akiwa na AC Milan, Bologna, Inter Milan na Brescia.

Alishinda taji la Ligi Kuu Italia, mara mbili, akiwa na Juventus na AC Milan. Baggio pia alitwaa tuzo ya Ballon d'Or mwaka 1993.

**#7. Michel Platini**

Michel Platini katika utawala wa soka mambo hayakwenda kama alivyotarajia, lakini uwanjani alikuwa mmoja wa wachezaji bora katika kipindi chake.

Platini alikuwa mmoja wa viungo washambuliaji bora zaidi akivaa jezi namba 10 akiwa na uwezo mkubwa wa kufunga mabao. Mfaransa huyo alianza kucheza soka akiwa na Nancy kabla ya kuichezea Saint-Etienne na Juventus.

Platini alishinda mataji mengi akiwa na Juventus, huku pia akitamba na timu ya Taifa ya Ufaransa na alishinda taji la Euro mwaka 1984.

Aidha, Platini alishinda tuzo ya Ballon d'Or mara tatu mwaka 1983, 1984 na 1985.

**#6. Ronaldinho**

Huyu ni mchezaji aliyeufanya mchezo wa soka kuonekana rahisi sana kwa namna alivyokuwa na madoido mengi uwanjani. Nyota huyu wa Brazil anajulikana kwa kile alichokifanya pale Barcelona.

Mchezaji wa daraja la juu kabisa kwa chenga za mauzi na alicheza jumla ya mechi 207 katika mashindano yote akiwa Barcelona, akifunga mabao 94. Pia alitoa mchango mkubwa zaidi kukua kisoka kwa Lionel Messi, ambaye ndiye mrithi wake hapo Barcelona wakati alipoondoka mwaka 2008. Ronaldinho alistaafu soka mwaka 2015 akitamba pia kwa AC Milan, Flamengo na Atletico Mineiro.

**#5. Zinedine Zidane**

Mmoja wa makocha wenye mafanikio makubwa duniani, Zinedine Zidane, ambaye kipindi chake cha uchezaji hakina tofauti sana na kwenye ukocha katika mafanikio.

Kiungo aliyekuwa na ubunifu na akili kubwa na alianza kucheza soka akiwa na Cannes na akatengeneza jina lake pale Bordeaux, na akahamia Juventus kwa dau la pauni milioni tatu mwaka 1996, kabla ya kwenda kufanya makubwa pale Real Madrid.

'Los Blancos' hao walilipa ada ya pauni milioni 70 ili kupata saini ya Zidane mwaka 2001. Sasa akiwa kocha wa Real Madrid, Zidane ameshinda mataji matatu mfululizo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na taji moja la LaLiga.

**#4. Zico**

Zico alitumia muda mwingi kucheza soka nchini Brazil, akiichezea Flamengo katika misimu miwili tofauti.

Nyota huyo wa zamani wa Brazil, alianza kucheza soka akiwa na Flamengo, akicheza mechi 506 katika mashindano yote na kufunga mabao 378 katika kipindi chake cha kwanza kuichezea klabu hiyo.

Zico mwenye umri wa miaka 68, alistaafu soka mwaka 1994, na kugeukia kwenye ukocha akizifundisha Fenerbahce, Bunyodkor, CSKA Moscow na Olympiacos. Pia alizifundisha timu za Taifa za Japan na Iraq. Kwa sasa ni mkurugenzi wa ufundi wa Kashima Antlers.

**#3. Pele**

Anachukuliwa na wengi kama mchezaji bora zaidi katika mchezo wa soka. Kama Zico, Pele pia alitumia muda wake mwingi kucheza soka nchini Brazil akiwa gwiji wa Santos, akicheza mechi 656 katika mashindano yote tangu alipoanza kucheza mwaka 1956 akifunga mabao 643.

Kwa Brazil, Pele alicheza mechi 92 akifunga mabao 77 na alishinda Kombe la Dunia akiwa na Brazil mwaka 1958, 1962 na 1970. Ni mfungaji wa wakati wote wa Brazil na Santos.

**#2. Lionel Messi**

Mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote wa Barcelona na Dunia, Lionel Messi, amefurahia mafanikio mengi zaidi katika soka. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina alianza kuichezea Barcelona mwaka 2004.

Messi amecheza mechi 774 katika mashindano yote kwa Barcelona (kabla ya mechi za jana), akifunga mabao 668 na kutoa pasi za mwisho 292. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 33, mkataba wake na Barcelona unafikia mwisho kipindi cha majira ya joto kinachokua na anahusishwa na Manchester City na Paris Saint-Germain.

**#1. Diego Maradona**

Mara zote kumekuwa na mlinganisho kati ya Lionel Messi na Diego Maradona na wote wana staili inayofanana kwenye soka.

Maradona anaheshima sana nchini Argentina licha ya kuwa na maisha ya ajabu nje ya uwanja kabla ya kifo chake.


Ni gwiji wa Napoli na alishinda Kombe la Dunia akiwa na Argentina wakati wa kipindi chake cha uchezaji.

Kama Messi, Maradona alikuwa na uwezo mkubwa wa kupiga chenga akitumia mguu wa kushoto. Kwa sasa Maradona jina lake ndilo linautambulisha Uwanja wa Napoli.


Maradona alifariki dunia Novemba, mwaka 2020 kwa mshituko wa moyo.

## Nukuu


"Hakuna ambaye anazungumza na mimi kuhusu mkataba, hivyo siwezi kusema zaidi, tusubiri na tuone, muda utazungumza kwa kuwa mimi sijui lolote lile," **mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah**



"Kila siku ninajifunza kutoka kwa Zinedine Zidane, katika kipindi cha mazoezi. Alikuwa mchezaji mkubwa na ni kocha mkubwa. Pia ananifanya kujiamini sana, na ninajifunza kila kitu chake uwanjani," **mshambuliaji kinda wa Real Madrid, Vinicius Junior**



"Kushinda mataji na klabu kunakusaini kupata uzoefu wa kutosha kwenye mechi za kimataifa, akili yangu ni kuhakikisha tunabeba taji na Ubelgiji, na hivyo ndivyo nilivyojiandaa kwa sasa. Hicho ni kitu nilichokikosa kwa kipindi kirefu kwenye maisha yangu ya soka. Nilishakata tamaa mara nyingi," **Romelu Lukaku baada ya kuipa Inter Milan ubingwa wa Serie A msimu huu, akieleza anavyolitaka taji la Euro 2020 akiwa na Ubelgiji**



# SIMBA, YANGA KUKIMBIANA NDIZO ZAO, HAIKUANZA J'MOSI

**Na Adam Fungamwango**

KITU ambacho hakikutegemewa na mashabiki wa soka nchini juzi, Jumamosi ni kushindwa kushuhudia mechi ya watani wa jadi Simba na Yanga iliokuwa ichezwe kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Badala yale mashabiki waliokuwa uwanjani walikutana na kadhia ya jua kali mchana na usiku mabomu, kutokana na baadhi yao kuchachamaa kutaka warudishiwe viingilio vyao.

Kashehe lilianza baada ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kusogeza muda wa mechi hiyo kutoka saa 11:00 hadi saa 1:00 usiku kwa kile walichoeleza ni kupokea maelekezo kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo.

Yanga haikukubaliana na hilo, ikapeleka timu saa 11:00 kama ilivyokuwa awali na baadaye wakaondoka. Ikatoa tamko kuwa yenyewe inasimimia Kanuni ya 15 (10) ya Ligi Kuu inayohusu taratibu za michezo ambayo inataka mabadiliko yote ya michezo yatajulishwa kwa pande zote husika angalau saa 24 kabla ya muda wa awali. Timu ya Simba iliwasili muda uliosogezwa ikidhaniwa kuwa inaweza kupata ushindi wa pointi tatu na mabao matatu, lakini muda mfupi baadaye, uwanjani hapo ikatangazwa kuwa mechi hiyo imeahirishwa.

Pamoja na utani wa jadi mechi hizi wakati mwingine huwa na siasa nyingi nje ya uwanja.

Kwenye makala haya tutaangalia baadhi ya matukio ambayo yalisababisha mechi hizo kuingia matatizoni, hasa zile ambazo zilipangwa kuchezwa na hazijachezwa kama juzi na moja ambayo ilichezwa kwa nusu ya kwanza tu, twende sasa...



Basi la wachezaji wa Yanga likitoka Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Jumamosi baada klabu hiyo kususia mechi dhidi ya Simba kwa madai ya kutokubaliana na mabadiliko ya muda wa mchezo kinyume cha kanuni, kutoka saa 11:00 hadi 1:00 usiku. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Simba kususa baada ya dakika 45**

Ilikuwa ni Agosti 10, mwaka 1985 wakati mechi ya Simba na Yanga ilipochezwa Uwanja wa Taifa, kwa sasa unaitwa Uhuru.

Mwamuzi wa mchezo huyo alikuwa ni Hadih Ali kutoka Zanzibar. Kilichoonekana uwanjani ni kwamba Simba iliamua kutembeza buti kweli kweli, lakini refa alionekana kutotoa kadi kwa wachezaji wa timu hiyo. Ikizidi sana anatoa njano. Mashabiki wa Yanga walichamaa majukwaani kuona hali hiyo. Yanga nayo ilionekana kama kuachiwa mipira mitatu ambayo walionekana wachezaji wake wameotea. Kwa bahati nzuri au mbaya walikosa kufunga kutokana kila mmoja kutaka kufunga yeye. Kipindi cha pili Simba haikurejea uwanjani na Yanga wakapewa ushindi wa pointi mbili na mabao mawili.

Viongozi wa Simba waliibuka na kudai walifanya hivyo kutokana na madai ya wachezaji wao kuwa mwamuzi alikuwa akiwaambia kuwa lazima wafungwe mechi hiyo. Na hata walipokuwa wakicheza rafu na mwamuzi kushindwa kuwapa kadi alikuwa akiwambia hatowapa kadi kwa sababu anataka wafungwe wakiwa wote wametimia, isionekane wameonewa. Hiyo ndiyo sababu Simba iliondoka uwanjani timu hizo zikiwa bado hazijafungana.

**Yanga yagoma, SMG kuambiwa si raia**

Mwaka 2001, kulizuka songombingo kama hili, baada ya Yanga kukataa kupeleka timu uwanjani kutokana na mchezaji wao tegemeo wakati huo, Said Maulidi kuambiwa kuwa si raia wa Tanzania.

Ikumbukwe mchezaji huyo alijiunga na Simba mwaka 1995 akitokea Mbanga ya Kigoma na kucheza ligi bila matatizo yoyote.

Lakini alipojiunga na Yanga mwaka 2001, zengwe lilitengenezwa, kwani siku chache tu kabla ya mechi ya watani ikatoka taarifa kutoka Idara ya Uhamiaji kuwa mchezaji huyo si raia wa Tanzania, hivyo hapaswi kucheza hadi taratibu zote za mchezaji wa kigeni zikamilishwe.

Yanga haikupeleka timu uwanjani na kilichotokea, kama ilivyokuwa juzi, mamlaka husika iliamua kuahirisha mechi hiyo na kupangiwa siku nyingine. Ilichezwa tena Septemba, Mosi 2001 wakati mchezaji huyo tayari ameshathibitishwa kuwa ni raia, Simba ikashinda bao 1-0 lililofungwa na Joseph Kaniki.

**Yanga kuikimbia Simba Kagame Cup**

Yanga haikwenda kucheza mechi iliyokuwa ichezwe Uwanja wa Taifa sasa Benjamin Mkapa dhidi ya Simba, kutafuta mshindi wa tatu michuano ya Kombe la Kagame.

Ilikuwa ni Julai 2008 michuano hiyo ilipofanyika nchini Tanzania. Simba ilifungwa bao 1-0 na URA ya Uganda na Yanga ikachapwa bao 1-0 dhidi ya Tusker ya Kenya kwenye hatua za nusu fainali.

Ilikuwa zicheze kutafuta mshindi wa tatu, lakini Yanga haikutia timu ikidai kuwa walikaa na Simba na kukubaliana kwanza walipwe Sh. milioni 50 na Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) kabla ya kucheza, lakini wanashangaa wenzao wamekiuka makubaliano hayo.

Tofauti na mechi ya juzi ambayo iliahirishwa, lakini ile ya mwaka huo waamuzi waliingia uwanjani na Simba ikapewa ushindi na kutwaa medali ya shaba, wakawa washindi wa tatu wa michuano hiyo.

**JE, WAJUA?**



KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, ni kocha wa kwanza kwenye historia ya michuano ya Kombe la Europa/ Ligi ya Mabingwa Ulaya kutinga fainali ya michuano hiyo mara mbili mfululizo akiwa na klabu mbili tofauti.



# Uchunguzi wa EWURA wabaini mambo 11

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imebaini mambo 11 katika uchunguzi wake wa malalamiko ya ankra za maji, huku ikipendekeza mamlaka za uteuzi kuzichukulia hatua za kinidhamu Mamlaka za Babati, Tanga na Kigoma ambazo zimekuwa sugu na kushindwa kutatua malalamiko hayo.

Miongoni mwa mambo yaliyobainika ni pamoja na ubambikizaji ambapo Mamlaka ya Maji Kigoma imeonekana kuwa kinara wa kubambikizia wateja ankra kwa asilimia 80 ya malalamiko, huku Babati na Tanga zikibainika kutoza wananchi bei juu zaidi ya zilizoidhinishwa na EWURA.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, alisema Mamlaka hiyo ilifanya ukaguzi maalum katika Mamlaka za maji 24 baada ya kusitisha utozaji wa bei mpya za maji zilizopaswa kuanza kutumika Januari 2021.

"Kutokana na malalamiko mengi kutoka kwa watumiaji wa huduma za maji nchini yakihusisha kubambikiwa bili, usomaji wa mita usiokuwa shirikishi na ukataji wa maji pasipokufuata kanuni na taratibu zilizowekwa, tuliamua kusitisha bei hizo ili kutoa nafasi kwa EWURA kufanya uchunguzi wa malalamiko hayo," alisema.

Mhandisi Chibulunje alitaja Mamlaka zilizofanyiwa ukaguzi huo ni pamoja na Kigoma, Bukoba, Babati, Moshi, Arusha, Tanga, Geita, Shinyanga, Kahama na Dodoma.

Nyingine ni Iringa, Musoma, Mbeya, Njombe, Songea, Vwawa-Mlowo, Mugango-Kiabakari, Bunda, Makambako, Sengerema, Muleba, Mwanhunzi, Gairo na Ngara.

Mkurugenzi huyo alisema baada ya uchunguzi huo EWURA ilibaini kuna udhaifu katika usomaji wa mita ambapo baadhi ya wasoma mita wanakosa umakini katika utekelezaji wa jukumu hilo.

"Tatizo hili limeonekana katika mamlaka zote 24 zilizofanyiwa uchunguzi, na kwenye uchunguzi huo Mamlaka ya Maji Kigoma ndio wanaongoza kwa kubambikizia bili ambapo asilimia 80 ya malalamiko yanahusu bili za maji,"alisema.

Aliongeza: "Kingine kilichobainika ni udhaifu katika mita za maji, baadhi ya mita zilibainika kutofanya kazi kwa ufanisi baada ya kuhakikiwa na Wakala wa Vipimo na Mizani (WMA).Tatizo hili limejionesha zaidi kwa mamlaka ya maji Iringa na Dodoma."

"Baadhi ya mamlaka kutoza bili za maji kwa kufanya makadirio kutokana na kuharibika kwa mita za maji, mfano mamlaka ya Tanga imeonekana inapeleka bili za makadirio kwa wateja, pia kuna uzembe wa baadhi ya mamlaka za maji katika usimamizi wa bei zinazotozwa kwa wateja," alisema.

Alitaja mamlaka ambazo zimebainika kutoza bei za juu za zile zilizoidhinishwa na EWURA kuwa ni Mbeya, Makambako, Songea, Tanga, Iringa, Shinyanga, Kahama, Geita, Arusha, Moshi, Babati, Ngara na Kigoma.

Mhandisi Chibulunje alisema kutokana na matokeo hayo imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kutoza faini ya Sh. 500,000 kwa mamlaka ya maji Tanga na Babati kwa kuwauzia wananchi maji kwa bei ambayo haijaidhinishwa na EWURA.

"Pia mamlaka zimeagizwa na EWURA kuwafidia wateja waliotozwa bili za maji zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa na EWURA,"

"EWURA imezipelekea maagizo mamlaka za maji za Mbeya, Songea, Makambako, Mwanhuzi na Gairo, zijieleze kwanini zisichukuliwe hatua stahiki kwa kukiuka maagizo ya EWURA, pia mwezi huu EWURA imeziandikia maagizo mamlaka za Geita, Kahama, Shinyanga, Iringa, Arusha, Moshi, Babati, Kigoma na Ngara ziache mara moja kutoza bei ambazo hazijaidhinishwa na EWURA kwenye magati,"alisema.

Hata hivyo, alisema EWURA itaendelea kufanya uchunguzi kwa mamlaka zingine zilizobaki na kuchukua hatua stahiki.

Naye, Kaimu Mkurugenzi wa Maji na Usafi wa Mazingira EWURA, Mhandisi Titus Safari, alisema mamlaka zilizofanyiwa ukaguzi huo ni kati ya 94 za mikoa, Miji ya Wilaya na Miji midogo.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratiu Ndejembi (kulia), akiwakabidi taulo za kike wanafunzi wa shule ya sekondari ya Dabalo iliyopo Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma jana . **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bil. 3.2/- kuwaendeleza wabunifu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imetoa Sh. bilioni 3.2 kwa ajili ya kuendeleza wabunifu wakiwamo 130 walioshinda kwenye Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) ya mwaka 2019 na 2020 ili bunifu zao zifikie hatua ya kutatua kero zilizopo kwa jamii.

Akizungumza jana kwenye uzinduzi wa mashindano hayo kwa mwaka huu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema pia serikali imefanya marekebisho katika mitaala ya kufundishia teknolojia za kidigitali, imeanzishwa kwenye taasisi za elimu ya juu ili kupatikana kwa wabunifu wengi.

Pia alisema kwa miaka mitano kutoka 2015 hadi 2020 wametambua wameendeleza teknolojia mbalimbali na miradi 215 imefadhiliwa na serikali katika kuhakikisha kuwa ubunifu unaibuliwa na kuleta manufaa kwa Watanzania.

Prof. Ndalichako alizitaka taasisi zote zinazohusika na kuibua ubunifu wa aina mbalimbali nchini kuongeza kasi katika kutambua ubunifu mpya katika ngazi mbalimbali ili nchi ijenge uwezo wa ndani bila kutegemea teknolojia za nje.

Alisema lazima taasisi zote zinazohusika na uibuaji wa bunifu za teknolojia lazima ziongeze kasi ya kuuibua na kuuendeleza ubunifu huo ili katika kuwezesha mapinduzi ya kiteknolojia katika sekta mbalimbali zikiwamo afya na kilimo.

"Natambua kuna mwongozo wa kuwatambua wabunifu katika halmashauri zetu kwa hiyo nawaelekeza msimamie kuhakikisha mwongozo ule unafanya kazi kwa sababu naamini tunao wabunifu wengi sana kuliko wale tunaowaibua kupitia MAKISATU,"alisema. Prof. Ndalichako.

Hata hivyo, alisema serikali imeanzisha vituo atamizi 17 nchini kwa lengo la kulea ubunifu wa teknolojia mbalimbali zilizowezesha kuanzishwa kwa kampuni 94 zilizotoa ajira 600 kwa Watanzania.

Pia alisema wameanzisha kumbi za ubunifu katika vyuo mbalimbali vikiwamo Chuo Kikuu cha Dar es saalam na Dodoma na taasisi ya sayansi ya Karume vyote ni kuhakikisha wanapanua wigo wa Watanzania kuendeleza ubunifu wao ili kuleta tija.

Awali, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk.Leonard Akwilapo, alisema mashindano hayo yalianzishwa mwaka 2019 na ni moja ya mikakati ya wizara ya kuibua na kutambua ubunifu wa teknolojia zinazovumbuliwa na Watanzania.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili jumla ya wabunifu 1066 wameibuliwa na kutambuliwa na wizara, na wabunifu mahiri 130 wanaendelezwa na wizara ambapo wanasimamiwa na taasisi mbalimbali.

"Bunifu 26 kati ya 130 zipo katika hatua ya kubiasharisha katika sekta mbalimbali, pia 83 zinaendelea kuboreshwa ili kufikia kwenye kubiasharishwa, na 21 zipo katika hatua ya awali kuelekea kuboreshwa."

"Wabunifu 714 wamejitokeza kushiriki katika makundi saba ambapo lengo ni kupata wabunifu 70, mchujo ulikuwa mkali sana, wabunifu hawa watashindanishwa kupitia tathmini itakayofanywa na majaji na tutapata wabunifu 21 ambao watatambuliwa na kupewa zawadi zao siku tutakayokuwa tunahitimisha," alisema.

Alisema taasisi 50 zinashiriki katika maonesho hayo ikiwamo wabunifu 24 walioshiriki mwaka 2019 na 2020 na wengi wao ni wale ambao bunifu zao zinaendelezwa na serikali.

# Ripoti ya ubunifu kupewa kipaumbele

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeahidi kuipa kipaumbele ripoti ya kimataifa ya ubunifu kwa kuwa ni kipimo cha taifa kwa wadau wanaotaka kuwekeza au kufanya biashara nchini.

Ripoti hiyo imeandaliwa na uratibu wa Shirika la Haki Miliki Duniani kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Cornel cha Marekani ambayo inaangalia hali ya nchi katika suala la ubunifu, uimara na udhaifu wa mfumo mzima wa ubunifu.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Juma Omary Kipanga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa kwenye ufunguzi wa warsha iliyoandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

Alisema ripoti hiyo imepima zaidi viashiria 80 katika nyanja mbalimbali kwenye elimu, miundombinu na uhalisi wa kufanya biashara.

"Nampongeza sana Katibu Mkuu, uongozi wa COSTECH na waandaaji wote kwa kutukutanisha hapa kujadiliana na kuweka mikakati ya pamoja kuhusu suala zima la kuipaisha Tanzania katika suala zima la ubunifu," alisema Kipanga.

Alibainisha kuwa katika ripoti hiyo imeonesha Tanzania imekuwa ikipata mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2020 imekuwa ni nchi ya nne

Kusini mwa Jangwa la Sahara nyuma ya nchi za Afrika Kusini na Kenya katika masuala ya bunifu.

"Bado kuna nafasi ya kuboresha na kupanda zaidi kwani nimejulishwa kuwa kuna maeneo hayakufanya vizuri kwa kuwa taarifa zilizotumika kuandaa hiyo ripoti hazikupatikana au zilizopatikana zilikuwa zimepitwa na wakati," alisema Kipanga.



## Uchimbaji visima vya majaribio jotoardhi rasmi

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

SERIKALI kupitia Kampuni ya uendelezaji wa Jotoardhi nchini (TGDC), imeanza kuchimba moja ya visima vitatu vya kufanyia majaribio ya uzalishaji wa Umeme kwenye Mradi wa Mbaka-Kyejo uliopo katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe.

Meneja Mkuu wa TGDC, Mhandisi Kato Kabaka, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kuhitimisha mafunzo ya kuwajengea uwezo wanahabari kutoka mikoa ya Mbeya na Songwe kuhusu uendelezaji wa vyanzo vya Jotoardhi nchini.

Alisema katika eneo hilo vitachimbwa visima vitatu ambavyo kila kimoja kitakuwa na urefu wa mita 300 sawa na viwanja vitatu vya mpira wa miguu na kwamba kwa sasa wameanza na kisima kimoja na wakimaliza watafuata vingine.

Alisema mpaka sasa kisima cha kwanza wamechimba na kufikia urefu wa zaidi ya Mita 70 na kwamba kazi hiyo inafanywa na wataalamu wa ndani ambao ni kutoka katika kampuni hiyo na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

"Kati ya maeneo yote ambayo kuna Jotoardhi, hapa ndipo tulipoamua kuanza uendelezaji na mradi huu utatumika kuzalisha umeme, kuvutia watalii na kutumia kwenye kilimo na ufugaji," alisema Mhandisi Kabaka.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa TGDC, Mhandisi Shakiru Kajugusi, alisema nishati ya Jotoardhi ni rafiki wa mazingira na ina faida kubwa kwa taifa kuliko hata nishati zingine.

Alisema uendelezaji wa Jotoardhi una gharama kubwa kwenye hatua za mwanzo ikiwemo utafiti na uchorongaji wa visima lakini baada ya hapo gharama zake huwa zinapungua.

Wandishi 27 kutoka katika mikoa ya Mbeya na Songwe walihudhuria mafunzo hayo kutokana na kuwa mikoa hiyo ni miongoni mwa maeneo yenye jotoardhi ambapo kwa Mkoa wa Mbeya yako mawili ambayo ni Ziwa Ngosi na Mbaka-Kyejo na kwa Mkoa wa Songwe inapatikana Songwe.

# Walimu matatani kwa madai ya kufanya mapenzi na wanafunzi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WALIMU wanne wa Shule ya Sekondari Isangawana wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kukutwa wakifanya tendo la ndoa na wanafunzi wa shule hiyo.

Walimu hao walikamatwa juzi na kuwekwa chini ya ulinzi kwa amri ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo iliyoongozwa na Mwenyekiti wake, Saimon Mayeka, ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya hiyo ilipotembelea shule hiyo kwa ajili ya kushughulikia tatizo hilo.

Walimu hao wanadaiwa kunaswa wakifanya vitendo hivyo kufuatiwa mtego waliokuwa wamewekewa na Mkuu wa Shule hiyo, Tipso Gideon na Ofisa Tarafa wa Tarafa ya Kipembawe wilayani humo, Kassim Kirandomala ambao ulifanikisha kumnasa mmoja wapo mbashara akiwa uchi wa mnyama na mwanafunzi chumbani wakifanya mapenzi.

Walimu wanaoshikiliwa ni Samson Njonanje, Ramadhan Shaban, Yose Elisalia na Dotto Salande ambaye ndiye anadaiwa kukamatwa mara ya mwisho akiwa na mmoja wa wanafunzi hao kwenye chumba cha nyumba inayomilikiwa na mmoja wa walimu hao.

Akizungumza mbele ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo, Mkuu wa Shule hiyo ya Isangawana, Mwalimu Gideon alisema vitendo hivyo vilianza kushamiri shuleni hapo mwaka jana na kwamba alipobaini alichukua hatua mbalimbali.

Alisema moja kati ya hatua alizozichukua ni pamoja na kuwaita walimu waliotajwa na kuandika maelezo yao kisha kuwapeleka kwenye Bodi ya Shule ili iwashughulikie kwa mujibu wa sheria.

Alisema Machi 18, mwaka huu, Bodi ya Shule iliwaita walimu hao na kuwachukulia hatua mbalimbali na kwamba baadhi walisamehewa isipokuwa mmoja ambaye ilielekezwa apelekwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kwa ajili ya hatua zaidi.

"Mimi kama Katibu wa Bodi nilielekezwa nimpeleke huyu mmoja kwa Mkurugenzi ili aondolewe hapa shuleni, lakini baada ya kupelekwa kwa Mkurugenzi akapandishwa na kupelekwa kuwa Mkuu wa Shule jirani ya Mtanila," alisema Gideon.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo ya Sekondari Isangawana, Lutangilo Nsemwa alisema tuhuma za walimu hao kufanya vitendo hivyo zilianza kubainika mwaka 2016, lakini walikuwa hawana uthibitisho ambao ungewasaidia kuwachukulia hatua.

Alisema walianza kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kuwaita walimu hao na kuchukua maelezo yao lakini bado waliendelea na uhuni huo na ndipo ikaanza kuandaliwa mipango ya kuwanasa.

Alisema wakati huo Mkuu wa Shule hiyo kwa sasa alikuwa bado hajapata wadhifa huo na kwamba tangu alipopatiwa nafasi hiyo bado hata miaka miwili haijakamilika, lakini ameshaanza kunyoosha nidhamu shuleni hapo.

Ofisa Tarafa wa Kipembawe, Kirandomala, ambaye ndiye aliyeshirikiana kuweka mtego wa kumnasa mmoja wa walimu hao alisema baada ya kuanza kufuatilia jambo hilo ulitokea mpasuko miongoni mwa walimu wa shule hiyo.

Alisema walimu hao walianza kumchukia mkuu wa shule na kuanza kutengeneza mizengwe ili kumharibia kazi hali ambayo ilianza hata kushusha taaluma ya wanafunzi wa shule hiyo.

"Tulipoanza kuchukua hatua hatukuangalia hata uwezo wao, kwa mfano huyu ambaye nyumba yake imekuwa ikitumika alikuwa anafanya vizuri sana kwenye somo lake, lakini Bodi iliamua kumchukulia hatua ya kumwazimia aondolewe lakini ndiyo akapandishwa cheo.

Baada ya maelezo ya viongozi hao, Mkuu wa Wilaya hiyo, Mayeka aliamuru Jeshi la Polisi kuwakamata walimu hao na kuwasweka ndani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria, huku akiwataka walimu wengine kuacha vitendo hivyo vinavyokinzana na miongozo ya kazi yao.

Aidha Mayeka aliagiza walimu hao wasimamishwe kazi mara moja wakati wakisubiri mkono wa sheria uchukuliwe dhidi yao.

"Hawa ni lazima watachukuliwa hatua, hatua zingine zinaanza kuchukuliwa leo kwanza wanasimamishwa kazi mpaka uchunguzi utakapokamilika na ikibainika ni kweli watafukuzwa kazi na kupelekwa mahakamani," alisema Mayeka.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi ambao walibainika kushiriki vitendo hivyo na walimu wao walilala selo kwa ajili ya kuwachukua maelezo ambapo wasichana 18 wa shule hiyo walibainika kuwa wameshafanyiwa vitendo hivyo na walimu hao wanne.




Mkurugenzi wa Benki ya Posta Tanzania (TPB), Sabasaba Moshingi, akizungumza jambo mwishoni mwa wiki, wakati benki hiyo ilipokuwa inalikabidhi Jeshi la Polisi nchini jengo la Kituo cha Polisi Wanamaji cha Itungi wilayani Kyela, jengo ambalo lilipokelewa na Kamishna wa Utawala wa Jeshi hilo nchini, (CP) Benedict Wakulyamba (wa pili kulia) kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, (IGP) Simon Sirro. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# TPB yakarabati jengo la Polisi

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

BENKI ya Posta (TPB) imekarabati Jengo la Kikosi cha Polisi Wanamaji-Itungi kilichopo wilayani Kyela Mkoa wa Mbeya ambalo lilikuwa limechakaa na kuanza kufifisha shughuli za ulinzi kwenye maeneo ya mwambao wa Ziwa Nyasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Sabasaba Moshingi, alikabidhi jengo hilo mwishoni mwa wiki na kupokelewa na Kamishna wa Utawala wa Jeshi la Polisi nchini, (CP) Benedict Wakulyamba ambaye alimwakilisha Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro.

Moshingi alisema ukarabati wa jengo hilo umegharimu Sh. milioni 48.6, na kwamba waliamua kulikarabati baada ya kupokea maombi ya jeshi hilo likidai kuwa jengo limechakaa kupita kiasi.

Alisema Jeshi la Polisi ni miongoni mwa wadau wa benki hiyo, ambao wengi wao huitumia kuweka fedha zao na kuchukua mikopo, hivyo hatua hiyo ni kurudisha fadhila kwa taasisi hiyo ili kuiongezea ufanisi katika utendaji kazi wa shughuli za ulinzi na usalama.

"Tutaendelea kutumia faida tunayopa, kurudi kwenye jamii yetu hivyo niwaombe tulitunze jengo hili, lakini, suala la miundombinu ya maji nitaenda kuangalia uwezekano wa kufanya hivyo na kurudi tena ili tulikamilishe," alisema Moshingi.

Akipokea Jengo hilo Kamishna wa Utawala wa Jeshi la Polisi, Wakulyamba, aliwatahadharisha wananchi na vikundi vya watu vinavyohatarisha amani ya nchi kwa kufanya matukio ya uhalifu akidai kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Aliwataka wananchi kutoa taarifa za siri endapo wataona kikundi ama mtu yeyote anayepanga kufanya uhalifu ili wadhibitiwe kabla hawajatekeleza uhuni wao.

Wakulyamba alisema Jeshi la Polisi halitakubali kuona kikundi au mtu yeyote bila kujali cheo au nafasi yake akijaribu kuvuruga amani na kwamba atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema amani ndio msingi wa maendeleo ya taifa lolote kwa maelezo kuwa bila amani watu hawawezi kufanya shughuli za uzalishaji mali na hivyo kufifisha maendeleo ya nchi. Alisema jeshi hilo halitakubali kuruhusu taifa liingie kwenye machafuko ya aina yoyote kwa kuwashughulikia wanaopanga kufanya matukio yanayohatarisha amani.

"Wadau wetu TPB wamejitokeza kuja kutuunga mkono ili kuboresha miundombinu ya Jeshi la Polisi ambayo itaongeza ufanisi katika utendaji kazi wetu, nitumie nafasi hii kuwaeleza kwamba wale wasiotaka kutii sheria kwa hiari tutawalazimisha," alisema Kamishna Wakulyamba.

Nae Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Kyela, (OCD), Ally Abubakar, alisema kikosi cha wanamaji Itungi kinatoa huduma za ulinzi na usalama katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Ruvuma kupitia Ziwa Nyasa.

Alisema jengo hilo lilijengwa 1974, lakini limekuwa likikarabatiwa mara kwa mara kutokana na uharibifu uliokuwa ukijitokeza lakini katika miaka ya hivi karibuni liliharibika zaidi kutokana na kukosa ufadhili wa kulikarabati.

Hata hivyo, alisema kutokana na jitihada za viongozi wa jeshi la polisi katika Wilaya ya Kyela na Mbeya kutafuta wadau wa kulikarabati walifanikiwa kupata ufadhili kutoka benki ya TPB ambao walianza kazi hiyo mwishoni mwa mwaka jana.





# SMZ, UNICEF kuendelea kuhifadhi haki za watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, imesema itaendelea kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) kuhakikisha huduma za afya zinaimarishwa hasa kulinda na kuhifadhi haki za watoto.

Hayo yalielezwa jana na Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, baada ya kukabidhiwa taarifa ya utafiti wa kiafya kutoka kwa Mwakilishi Mkaazi wa UNICEF Tanzania, Shalini Bahuguna.

Taarifa hiyo ilielezwa kwamba watoto wengi Zanzibar wamekuwa wanakosa haki zao za msingi, kutokana na kufanyiwa vitendo viovu, jambo ambalo linarejesha nyuma jitihada za kuwalinda.

Waziri huyo alisema katika taarifa ya utafiti huo, UNICEF imebaini kuwa Zanzibar kuna upungufu wa watendaji kwa baadhi ya vitengo na ameishauri wizara kuhakikisha inajaza nafasi za watumishi waliostaafu ili kutoa huduma kwa ufanisi kwa wagonjwa.

Aidha, taarifa ya UNICEF imeshauri kuimarishwa kitengo cha kinga ili kuwakinga wananchi na maradhi ya mlipuko na kuisistiza kuhamasisha wananchi kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na maradhi, ikiwamo kunawa mikono mara kwa mara, kuvaa barakoa na kuendeleza utaratibu wa kukaa kwa kupeana nafasi ambao unaonekana kusahaulika. Naye Mwakilishi wa UNICEF, Shalini Bahuguna, alisema kuwa Zanzibar bado kuna tatizo la upungufu wa damu kwa wajawazito hasa katika maeneo ya Micheweni Pemba, jambo ambalo linazorotesha afya ya mama na mtoto na ameitaka wizara ya afya kushughulikia suala hilo ili kuiweka jamii katika hali nzuri ya kiafya.

Mwakilishi huyo aliwataka Watanzania kuendelea kuchukua jitihada zaidi katika kuimarisha usafi wa mazingira pamoja na kuhakikisha wanakunywa majisafi na salama ili kulinda afya zao.

Waziri Mazrui alimhakikishia Mwakilishi huyo wa UNICEF itayafanyia kazi mapendekezo yote yaliyotolewa na shirika hilo katika kuhakikisha wananchi wanapatiwa huduma bora za afya mjini na vijijini.



Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, akisalimiana na Mwakilishi Mkaazi wa UNICEF nchini, Shalini Bahuguna, alipofika ofisini kwake mwishoni mwa wiki. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sheria kandamizi kwa wanahabari sasa kupitiwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Khamis Abdallah Said, amewataka waandishi wa habari habari Visiwani Zanzibar kupeleka mapendekezo yao kwa sheria ambazo wanaziona ni kandamizi kwao.

Alisema Wizara ipo tayari kuzifanyia mapitio baadhi ya sheria hizo ili waandishi wa habari kuwa huru na kufanya kazi zao bila ya vikwazo.

Naibu Katibu Mkuu huyo aliyasema hayo katika mkutano wa kuadhimisha Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari ulioendeshwa kwa njia ya mtandao wa zoom.

Alisema mabadiliko katika sekta ya habari yanaweza kutokea endapo waandishi wa habari watakua wamoja na weledi katika utendaji kazi zao.

Alisema kuwa yote hayo yataweza kutokea ikiwa waandishi wa habari hawatokubali kugawiwa ili kulinda heshima yao.

"Serikali imesikia kilio chenu, na sasa imetoa ruhusa ya kupeleka mapendekezo ya sheria na sera zenye mapungufu,"alisema.

Alieleza kuwa licha ya kuwapo kwa changamoto za kisheria, lakini haiwezekani kuachiwa watu kufanya wanavyotaka.

Alsema ni wakati kwa waandishi wa habari kutumia fursa ya wadau wa habari kuziainisha sheria ambazo wanaona zinahitaji kufanyiwa marekebisho badala ya kukaa tu na kulalamika.

"Suala la kulalamika litakuwa historia kama mtachukua hatua stahiki, masuala ya kuzungumza na kulalamika sasa hivi ni lazima mfanye kwa vitendo na tumieni fursa hii ambayo ni nzuri kwenu badala ya kulalamika... na sisi kama Serikali tutajitahidi kuhakikisha haki za waandishi wa habari zinalindwa," alisema.

Aidha, aliwataka waandishi wa habari kujitahidi kuandika habari ambazo zinagusa jamii na zenye tija kwa taifa pamoja na kujiendeleza kielimu.

Akitoa madaka katika mkutano huo, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk.Mzuri Issa, alisema kuwa waandishi wa habari wanawake wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Alisema katika vyombo vya habari kumetawaliwa na mifumo dume ambapo bado wanawake hawapewi nafasi za uongozi licha ya kuwa wanaelimu sawa na wanaume.

"Bado idadi ni ndogo ya wanawake viongozi katika vyombo vyetu vya habari licha ya kuwa wanawake wana uwezo mzuri na mahodari wa kufanya kazi," alisema Dk. Mzuri.

Washiriki wa mkutano huo walisema kuwa wakati umefika sasa kwa waandishi wa habari kuwa kitu kimoja ili tasnia hiyo kuheshimiwa.

"Tutapokuwa kitu kimoja tasnia yetu itaheshimika, lakini tusipokuwa wamoja, watu wabaya watapata mwanya wa kuivuruga na kuonekana hatuna thamani," alisema Hassan Issa, mwandishi wa habari mwandamizi.

## Idadi ya watoto wanaozaliwa njiti yaongezeka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

DAKTARI wa magonjwa bingwa wa watoto kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dk. Angostine Massawe, amesema idadi ya watoto njiti wanaozaliwa imeongezeka duniani, ambapo watoto milioni 15 huzaliwa kila mwaka.

Aliyasema hayo alipokuwa akitoa mafunzo kwa Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja huko.

Alisema watoto hao milioni moja hufariki dunia kila mwaka kutokana na matatizo mbalimbali wakati wa kuzaliwa na wanaofanikiwa kuishi hupata ulemavu wa kudumu .

Alisema kupata mtoto njiti inatokana na sababu mbalimbali ikiwamo ndoa za mapema ambapo mwanamke anapoolewa akiwa hajafikia umri wa miaka 19 anapopata ujauzito inachangia kuzaa mtoto njiti.

Alisema katika nchi za kipato cha chini asilimia 50 ya watoto wanaozaliwa kamili au kabla ya majuma 32 hufariki, kutokana na kukosa huduma muhimu zaidi ikiwamo joto, kunyonya na huduma muhimu dhidi ya maambulizi ya kupumua kwa shida.

Alisema kwa kuwa tatizo la watoto njiti limekuwa kubwa, aliitaka jamii ibadilike katika mtazamo wa ndoa za mapema chini ya umri wa miaka 17.

Aidha, aliwataka kinamama wanapojigundua kuwa na ujauzito kwenda hospitali ili kupata maelekezo ya madaktari mapemba kabla ya kusubiri ujauzito kuwa mkubwa.

Akifungua mafunzo hayo Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) taifa ambae pia Waziri wa Habari, Vijana, Sanaa na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema mafunzo hayo sasa yatakuwa endelevu kwa Zanzibar nzima ili elimu hiyo kuwafikia wanawake na kuepukana na changamoto za uzazi ambazo zinaepukika .

Alisema wanashiriana na wizara ya afya ili kuhakikisha kuwa maendeleo yote ya mji wa Zanzibar elimu ya mtoto njiti inawafikia hasa maeneo ya vijijini.

Washiriki wa mafunzo hayo, walisema elimu hiyo ni muhimu sio kwa wanawake pekee hata kwa wanaume kwa sababu baadhi ya jamii ina dhana kuwa kuzaa mtoto njiti ni kama mkosi katika familia, na wengine hupeleka imani zao katika mambo ya kishirikina.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MARGRETH ELIAS MAYALLA** anatangaza kupotelewa na CHETI CHA KIDATO CHA NNE yenye **No S.0224.0057** kilichotolewa na KIFUNGILO GIRLS SECONDARY SCHOOL mwaka 2010. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **REF:MW/RB/7988/2017.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LETICIA MBESA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC.559 CHR**, aina ya SANLG, yenye Chassis no.**LBRSPJB58K9004942,** Engine no. **SL157FMI19903692.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya jeshi la polisi. **SEG/RB/TR/199/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA ILEMELA**
**MADAI YA RUFAA NO 0 OF 2020**

**(Linatokana na shauri asilia la madai no 10/2020 kutoka mahakama ya mwanzo ilemela)**

**DAUDI MAGESA..............................MRUFAANI**
**DHIDI YA**
**1. ABITCH JOHN KASARE............MJIBU MAOMBI**
**2. ANNETH ELIAS.......................MJIBU MAOMBI**

**KWA:ANNETH ELIAS**
**WA KILIMAHEWA**
**P.O.BOX**
**ILEMELA- MWANZA**
**O719711560 AU POPOTE ULIPO TANZANIA BARA**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muomba rufaa amefungua shauri la rufaa ambalo limepangwa kutajwa tarehe 10/05/2021 mbele ya Mh .A.N.Sumari.
Hivyo basi unatakiwa kuhudhuria bila kukosa au mwakilishi wako Ili kusikiliza rufaa tajwa hapo juu.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 27 mwezi APRILI 2021.

..........................................................
**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA WILAYA ILEMELA**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA**
**AT BUKOBA**
**LAND APPEAL NO. 40/2020**
**(Arising from land application no. 6/2019 Bukoba District land and housing tribunal of Bukoba)**
**NATIONAL MICROFINANCE BANK BUKOBA PLC...............APPELLANT**
**VERSUS**
**1. SAIDA AMANYA SAID AND ANOTHER .........................RESPONDENT**
**2. VEDASTO KAJUNA ...............RESPONDENT**
**TO, VEDASTO KAJUNA**
**KEMONDO WARD, BUKOBA**
**RE: NOTICE FOR DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Appellant has lodged a case registered as land appeal no. 40/2020 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.
Take notice that the above said case has been schedualed for mention on 18th day of May, 2021 at 09:00 am before Hon. Judge F. H. MTULYA. You are authorized to appear in person or through your Advocate.
Take further notice that in default of your appearance on that date and time for said mention the case will proceed in your absence.
Give under my hand and seal of the court this 3rd day of May, 2021.

..........................................................
**J.M. MINDE**

**TANZANIA AGRICULTURE SOCIETY(TASO)**
**TASO KANDA YA KATI**

+2550623005799 06.05.2021.
+255768315145

**TANGAZO**

NOTICE YA SIKU THELATHINI (30) WA WAPANGAJI WOTE WALIOPANGISHA MAENEO(PLOTS)KATIKA KIWANJA CHA MAONYESHO YA KILIMO CHA NANENANE KILICHOPO KATA YA NZUGUNI KATIKA JIJI LA DODOMA

NDUGU WAPANGAJI, MADA TAJWA HAPO JUU YAHUSIKA, CHAMA CHA KILIMO TANZANIA(TASO) KANDA YA KATI KINAWAOMBA WAPANGAJI WAKE WOTE KUTEKELEZA YAFUATAYO;

1. KULIPA KODI ZA VIWANJA KWA MUDA WOTE AMBAO HAMJALIPA.
2. KUHAKIKISHA MNATIMIZA MASHARTI YOTE YALIYOMO KWENYE MIKATABA YENU NA TASO(OFFER)

ENDAPO MUDA ULIOTOLEWA HAPO JUU UTAPITA, CHAMA KITAWACHUKULIA HATUA ZA KISHERIA IKIWEMO KUWAPATIA MAENEO HAYO WAPANGAJI WENGINE.

TUMETOA TANGAZO HILI KWAKUA WENGI WENU HAMAPATIKANI KWENYE MAENEO YENU/KWA NJIA ZA KAWAIDA.

**TUNAWATAKIA UTEKELEZAJI MWEMA.**
**WENU KATIKA UJENZI WA TASO NA NCHI YETU KWA UJUMLA.**

HERRY HUSSEIN BEJI
KATIBU TASO KANDA YA KATI

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**IBRAHIM SHABAN MLOLWA**
anatangaza kupotelewa na passport ya kusafiria yenye namba za usajili TAE310191 iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani ya nchi DAR ES SALAAM mwaka 2020,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/MSI/RB/235304/2021**

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

**AAGAM TRADING LIMITED**
**P O BOX 59 SHINYANGA**
**BOARD RESOLUTION**

**SHAREHOLDERS RESOLTUION APPROVING DISSOLUTION OF THE COMPANY**

Name of company **AAGAM TRADING LIMITED** registered address **P O BOX 59** Shinyanga .
At a meeting of the Directors held at 09:00 am 15th March 2021. The following resolution was passed.

The shareholders of the company hereby dissolve the company with effect from 30th April 2021.

**NOW THEREFORE BE IT RESOLVED** that, the company shall wind up it affairs,and the company shall be dissolved

**Dated this 15th day of March 2021.**

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wanafunzi 50 wauawa katika mlipuko wa bomu

**Kabul, AFAGHANSTAN**

MLIPUKO wa bomu karibu na shule ya wasichana katika Wilaya ya Washia ya Magharibi ya mji mkuu Kabul, umeua wanafunzi ni 50 wengi wakiwa ni wasichana wenye umri kati ya miaka 11 na 15.

Aidha takriban 100 wamejeruhiwa, taarifa iliyothibitishwa na Polisi, Afghanistan, jana.

Haikufahamika mara moja kilichosababisha mlipuko huo, licha ya taarifa zinazopingana juu ya kilichosababisha mlipuko.

Awali baadhi ya vyombo vya habari vya viliripoti juu ya kutokea milipuko mitatu, iliyosababishwa na roketi, ripoti zingine zilidokeza kuwa mlipuko huo ulisababishwa na bomu lililolipuka kutoka kwenye gari.

Rais wa Afghanistan, Ashraf Ghani, aliwalaumu wapiganaji wa kundi la Taliban kwa shambulio hilo na kusema kundi hilo linaonyesha kuwa halina nia ya kuutatua mgogoro wa nchi hiyo kwa amani.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Tariq Arian, alisema idadi ya vifo inatarajiwa kuongezeka baada ya shambulio hilo la bomu liliyotokea katika kitongoji cha Dasht-e-Barchi kwenye eneo la Shule ya Syed Al-Shahda na kwamba watu wapatao 55, waliojeruhiwa walipelekwa kwenye hospitali mbalimbali kwa ajili ya matibabu.

Shirika la Uingereza linaloshughulikia hali za dharura na ambalo linaendesha kutoa matibabu mjini Kabul, lilisema limepokea watu 26 waliojeruhiwa kwenye mlipuko huo.

Taarifa zaidi zilisema kwamba mlipuko huo ulitokea wakati wakazi wengi walipokuwa wakifanya ununuzi katika maandalizi ya kuelekea sikukuu ya Eid-al-Fitr.

Eneo hilo linalokaliwa kwa kiasi kikubwa na jamii ya washia wa Hazara, limekuwa likilengwa na wanamgambo wa Kisunni.

Juhudi za kutafuta amani kati ya serikali ya Afghanistan na kundi la Taliban ili kumaliza vita vya miongo kadhaa zimekuwa zikilegalega.

Shambulio hilo la bomu linaongeza hofu kwamba vurugu katika nchi ya Afghanistan, iliyokumbwa na vita zinaweza kuongezeka wakati Marekani na NATO zinaazimia kuyaondoa majeshi yao baada ya kukaa nchini humo kwa miaka 20.

Balozi wa Marekani nchini Afghanistan, Ross Wilson, alisema kwenye Twitter kwamba shambulio hilo ni kitu cha kuchukiza na ni unyama dhidi ya binadamu wasio na hatia.

"Asili ya mlipuko wa bomu hili ni kifaa kilichofungwa kwenye gari," Msemaji wa Polisi mjini Kabul, Ferdaus Faramarz aliwaambia waandishi wa habari kupitia ujumbe mfupi wa maandishi.

***DW/AP***



Watu wakishuhudia mali za wanafunzi ambao waliuawa kwa bomu mjini Kabul, nchini Afghanstan, jana. Inakadiriwa vifo vilifikia 50 wengi wao wakiwa ni wasichana wenye umri kati ya miaka 11 na 15 . **PICHA: XINHUA**

# Wanajeshi 16 wauawa katika maandamano dhidi ya jeshi

**Yangon, MYANMAR**

WANAJESHI wasiopungua 16 wameuawa kwenye mapigano kati ya waandamanaji na jeshi la mapinduzi Myanmar.

Waliuawa katika mapigano kati ya jeshi la mapinduzi na waandamanaji yaliyotokea wiki hii.

Kulingana na ripoti iliyotolewa katika gazeti la The Irrawaddy, wakati wa maandamano ya Mei 6 na 7, mwaka huu, katika wilaya ya Kani ya Jimbo la Sagaing, waandamanaji walikabiliana na jeshi kwa silaha za mikono baada ya kutumia silaha kutawanya umati. Wanajeshi wasiopungua 16 waliuawa katika mapigano hayo yalitokea.

Inasemekana kwamba wale ambao walijibu makabiliano ya jeshi la Myanmar walikuwa washiriki wa kundi lenye silaha linalojiita vikosi vya raia.

Kwa upande mwingine, idadi ya raia waliofariki kutokana na makabiliano ya silaha ya jeshi la katika maandamano hadi sasa imefikia watu 774, tangu yafanyike mapinduzi Februari Mosi, mwaka huu.

Katika ripoti ya kila siku ya Chama cha Msaada wa Wafungwa wa Kisiasa (AAPP), iliripotiwa kuwa majeruhi wawili zaidi walithibitishwa kutokea ndani ya saa 24 zilizopita.

Katika ripoti hiyo, pia ilielezwa kwamba kulikuwa na vibali vya kukamata watu 1,498.

***TRT***

## Jumuiya kimataifa zahofia ghasia zikiendelea Jerusalem

**Washington, MAREKANI**

JUMUIYA ya kimataifa, imeelezea wasiwasi mkubwa juu ya ghasia zinazoendelea mjini Jerusalem, siku moja baada ya makabiliano baina ya polisi wa Israel na Waplestina.

Ghasia hizo zilisababisha watu zaidi ya 200 kujeruhiwa.

Taarifa ya pamoja iliyotolewa na Marekani, Urusi, Umoja wa Ulaya (EU) na Umoja wa Mataifa (UN), zilisema kusikitishwa na kauli za uchochezi zilizotolewa na baadhi ya makundi ya kisiasa, pamoja na kurushwa kwa roketi.

Aidha taarifa hiyo pia ililaani kuanza tena urushaji maputo ya moto kutoka upande wa Gaza, kuelekea Israel pamoja na kushambuliwa mashamba ya Wapalestina katika Ukingo wa Magharibi.

Licha ya kutolewa miito ya kimataifa, ghasia ziliendelea, huku watu wengi wakijeruhiwa wakati polisi wa Israel walipofyatua maji ya kuwasha na risasi za mipira kutawanya wandamanaji wa Kipalestina katika eneo la Jerusalem Mashariki.

***DW***

## Iran kutoa ushirikiano kwa wakaguzi wa IAEA

**Vienna, AUSTRIA**

OFISA Mwandamizi wa Iran, amesema nchi yake itaongeza ushirikiano na Shirika la Nishati ya Atomiki Duniani (IAEA), juu ya ukaguzi wa vituo vyake vya nyuklia.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Abbas Araghchi alizungumza hayo na shirika habari la NHK jijini Vienna nchini Austria, mwishoni mwa wiki.

Naibu huyo anaongoza ujumbe wa Iran kwenye majadiliano yasiyo ya moja kwa moja na Marekani yanayoendelea sasa kwenye mji huo mkuu wa Austria.

Iran iliashiria kuwa ipo tayari kuhitimisha ushirikiano wake na IAEA, kuhusu ukaguzi iwapo hakutafikiwa maendeleo yoyote kwenye majadiliano kuhusiana na Marekani kuiondolea nchi hiyo vikwazo na masuala mengine hadi kufikia mwishoni mwa Mei.


Araghchi, alimweleza mwandishi wa habari wa NHK kuwa Iran inatumai maendeleo ya kutosha yatafikiwa ili kusiwepo na hitaji la kuongeza ukaguzi.

Alisema kuwa iwapo hatua hiyo itahitajika, Iran itaangazia kuongezwa huko kufanyike katika wakati mwafaka.

Mwezi uliopita, Mkurugenzi Mkuu wa IAEA, Rafael Grossi, alisema shirika hilo huenda likahitaji kujadili tena suala hilo na Iran, iwapo hakuna makubaliano yoyote yatakayofikiwa miongoni mwa watia saini wa makubaliano ya nyuklia ya mwaka 2015.

Araghchi na Grossi, wanaaminika kuwa walijadiliana juu ya suala hilo, walipokutana Alhamisi ya wiki iliyopita, kwenye makao makuu ya IAEA, jijini Vienna.

***NHK***






## RAMOS AKUMBWA NA JERAHA JIPYA

**MADRID, Hispania**

NAHODHA wa Real Madrid, Sergio Ramos, anakabiliwa na jeraha lingine ambalo litamuweka nje hadi mwisho mwa msimu huu.

Ramos alicheza mchezo wake wa kwanza kwa Real Madrid dhidi ya Chelsea kwenye nusu fainali ya pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuwa nje ya dimba kwa wiki saba.

Madrid walitupwa nje kwenye michuano hiyo, baada ya kukubali kipigo cha mabao 2-0.

Lakini sasa amerudi tena benchi baada ya kupata jeraha lake la tatu kwa msimu huu, alikosa mazoezi Jumamosi kuelekea mchezo mkubwa dhidi ya Sevilla jana Jumapili.

Taarifa ya klabu ilisomeka: "Baada ya vipimo vilivyofanywa na timu ya matibabu kwa mchezaji Sergio Ramos anakabiliwa na jeraha la misuli katika mguu wake wa kushoto, hivyo matibabu yake yataendelea kufuatiliwa kwa karibu."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, anaeleka kumaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu huu na bado hajakubali kuongeza mkataba mpya.

# ARSENAL YAWANIA KUMSAJILI ONANA

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal imeingia kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinda mlango wa Ajax, Andre Onana, kipindi cha majira ya joto msimu huu, lakini watasubiri uamuzi katika rufaa yake ijayo dhidi ya marufuku ya kutumia dawa za kulevya kabla ya kumsajili.

Onana kwa sasa anatumikia adhabu ya kusimamishwa kwa miezi 12 aliyopewa na Shirikisho la Soka Ulaya (UEFA), baada ya kupatikana na hatia ya matumizi ya dawa iliyokatazwa ya Furosemide katika sampuli yake ya mkojo.

Kwa sasa amekata rufaa ya marufuku hiyo katika Mahakama ya Usuluhishi ya Michezo (CAS), na itasikilizwa mapema Juni, na uamuzi utatplewa baadaye mwezi huo.

Mawakili wa Onana wanaamini marufuku hiyo, ambayo kwa sasa inatakiwa kudumu hadi Februari 2022, inaweza kupunguzwa hadi miezi nane.

Ajax inataka kupokea karibu pauni milioni 12 kwa mlinda mlango huyo msimu huu wa joto, ikiwa rufaa yake itafanikiwa.

Lakini, ikizingatiwa kuwa mkataba wake unamalizika mwaka 2022, inawezekana ofa ikapungua mpaka pauni milioni saba na kufanya biashara na Arsenal.

## CHAMBERLAIN YUPO KWENYE MPANGO WANGU - KLOPP

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amekanusha kuondoka kwa kiungo Alex Oxlade-Chamberlain, ambaye bado ni sehemu ya mipango yake kwa msimu ujao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye alikosa miezi minne ya kwanza ya msimu huu baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti, amekuwa na msimu mgumu wa 2020-21 kwa 'Wekundu' hao na ameshindwa kujiimarisha na kujihakikishia nafasi kwenye kikosi cha kwanza.

Liverpool wamejipanga kuimarisha kikosi chao katika kipindi hiki cha usajili wa majira ya joto, ambapo inaweza kumaanisha mchezaji mmoja au wawili wa sasa wakalazimika kuondoka klabuni hapo.

Hata hivyo, Klopp amesema kuwa Oxlade-Chamberlain ni sehemu ya mipango yake ya msimu ujao.

"Wanaelewa hali hiyo ni wazi, lakini tunatumaini kuwa hiyo itabadilika kabisa msimu ujao kwa sababu ukiwa na utulivu zaidi katika safu ya mwisho basi unaweza kuwa na busara zaidi," alisema Klopp akinukuliwa na BT Sport.

"Je! Ninamtegemea kwa msimu ujao? Ndiyo. Yupo kwenye mipango yangu."

Oxlade-Chamberlain amecheza mechi 14 tu kwa Liverpool katika mashindano yote hadi sasa msimu huu, akianza mara mbili tu kwenye Ligi Kuu England.



HABARI MICHEZO



# BEI YA HAZARD NI EURO MILIONI 50 - MADRID

MADRID, Hispania

KLABU ya Real Madrid imetangaza kwamba, ipo tayari kumuuza kiungo wake, Eden Hazard kwa euro milioni 50 mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 alifunga mara nne tu katika mechi 40 kwa Real Madrid chini ya Zinedine Zidane tangu kuhamia kwake klabuni hapo akitoka Chelsea msimu wa 2019.

Hazard amepambana na shida kadhaa za majeraha wakati wake hapo kwenye dimba la Bernabeu, na ripoti ya hivi karibuni inadai kuwa 'Los Blancos' hao wanataka kumuuza katika dirisha la uhamisho wa majira ya joto.

Kwa mujibu wa ABC, Real Madrid itakuwa tayari kumruhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji aondoke ikiwa watapokea ofa kiasi cha kitita cha Euro milioni 50.

Hazard alipata shida kupata chochote dhidi ya Chelsea kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano usiku na kisha akapigwa picha akicheka na wachezaji wenzake wa zamani baada ya filimbi ya mwisho kule Stamford Bridge.

Nyota huyo wa zamani wa timu ya Lille ya Ufaransa, alicheza mechi 18 tu kwenye mashindano yote wakati wa msimu wa 2020-21 na amefunga mabao matatu tu.

# INTER MILAMI YATIA MGUU KWA YOUNG

MILAN, Italia

MLINZI wa Inter Milan, Ashley Young, anawaniwa na klabu ya Inter Miami inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani (MSL), kwa mujibu wa Sky Sport Italia.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, amekuwa na kiwango cha kuvutia kule Inter ambapo wametwaa ubingwa wa Ligi Kuu Italia, Serie A.

Beki huyo ambaye amewahi kucheza pia ndani ya Klabu ya Manchester United, majaliwa yake bado hajajulikana hapo Inter inayonolewa na kocha Antonio Conte.

Kutokana na uwezo wa nyota huyo, anatajwa kuiacha timu yake msimu utakapofika mwisho.



Inter Miami inayomilikiwa na nyota wa zamani wa Man United, David Beckham, Marcelo Claure na Jorge Mas, ipo tayari kushindana na Watford ili kupata saini ya nyota huyo.

Young aliwahi kucheza ndani ya Watford msimu wa 2003/2007 na alicheza jumla ya mechi 110 kabla ya kujiunga na Aston Villa kwa dau la euro milioni 9.65 msimu wa 2007.

# ARTETA KUENDELEA KUPETA ARSENAL

LONDON, England

ARSENAL haina mpango wa haraka wa kumtimua Kocha Mkuu, Mikel Arteta, kabla ya kuanza kwa msimu ujao.

Shinikizo linaanza kuongezeka kwa Arteta, baada ya timu yake kutofuzu nusu fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Villarreal.

'Washikabunduki' hao walipata sare ya bila kufungana pale Emirates, ambayo ilitosha kuwashuhudia 'Wana-LaLiga' walipo chini ya kocha wa zamani wa Arsenal, Unai Emery wakisonga mbele kwa jumla ya mabao 2-1.

Kwa mujibu wa Daily Mail, uongozi wa Arsenal hauamini kuwa mabadiliko ya kocha ni muhimu wakati huu, hasa baada ya msimu usio wa kawaida wa 2020-21 ambao uliathiriwa na mlipuko wa virusi vya corona.

Hata hivyo, bodi ya Arsenal imesikitishwa kwamba klabu haijafanya kwa kiwango kinachotarajiwa muhula huu na wanatarajia maboresho makubwa msimu ujao.

Ikiwa Arteta atabaki na kuwajibika zaidi ya msimu huu, mwanzo mbaya wa msimu wa 2021-22, utaweka hatiani kibarua cha kocha huyo mwenye umri wa miaka 39.

Mmiliki wa Arsenal, Stan Kroenke, ambaye anasisitiza kuwa klabu haiuzwi, atahakikisha kuna fedha zinazopatikana kwa msimu ujao, lakini mipango yao ya kusajili inategemea sana iwapo anaweza kupata nafasi ya kufuzu kwa Ligi ya Europa.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND SASA SOKONI KWA PAUNI MILIONI 150

●●●Manchester United, Manchester City, Real Madrid, Barcelona na Chelsea ni kati ya klabu zinazotajwa...

**DORTMUND, Ujerumani**

KLABU ya Borussia Dortmund imeripotiwa kuwa itakuwa tayari kumruhusu Erling Braut Haaland kuondoka klabuni hapo wakati wa dirisha la uhamisho la msimu huu wa joto ikiwa watapokea ofa ya angalau pauni milioni 150.

Hatma ya Haaland hapo Dortmund inaendelea kutiliwa shaka, huku Manchester United, Manchester City, Real Madrid, Barcelona na Chelsea zikiwa ni kati ya klabu zinazotajwa kuvutiwa naye.

Kwa mujibu wa Sky Sports, wababe hao wa Ujerumani hawatamuuza mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway kwa chini ya pauni milioni 150 na hawatakubaliana na wakala wa Haaland, Mino Raiola.

Ripoti hiyo inadai kwamba, Dortmund itawekwa katika wakati mgumu ikiwa watashindwa kupata nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu wa 2021-22.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, amekuwa tena katika kiwango bora katika klabu hiyo msimu huu, akifunga mara 37 na kutoa pasi za mwisho 11 katika mechi 38 za mashindano yote.

## KWA UFUPI

**LEWANDOWSKI AWANIWA EPL**
MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 32, anang'anganiwa na Chelsea na Manchester City. **(Mail)**

**SALAH ATAKIWA CHELSEA**
CHELSEA pia imemuongeza mshambuliaji wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 28, katika orodha yao inapojiandaa kuimarisha safu yake ya mashambulizi msimu huu wa joto. **(Bild Journalist, Christian Falk on Twitter)**

**NEYMAR KUBAKI PSG**
NYOTA wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 29, jana alitarajiwa kusaini mkataba wa kurefusha muda wake pale Paris St-Germain , hatua itakayomfanya kusalia katika klabu hiyo hadi mwaka 2026. **(L'Equipe)**

**MADRID KUMUUZA HAZARD**
KLABU ya Real Madrid imechoshwa na Eden Hazard na iko tayari kumuuza mshambuliaji huyo wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 30, msimu huu wa majira ya joto. **(Marca)**

**MOURINHO AMTAKA DE BEEK**
KOCHA mpya wa AS Roma, Jose Mourinho, ana mpango wa kubisha hodi katika klabu yake ya zamani ya Manchester United kwa lengo la kumnunua kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 24. **(Calciomercato)**

**SPURS KUTOMUUZA KANE**
TOTTENHAM Hotspur haina mpango wa kupokea ofa yoyote ya kumuuza mshambuliaji wake, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, msimu huu wa joto. **(Standard)**

**VILLA KUMSAJILI MCNEIL**
ASTON Villa inajiandaa kuwasilisha ofa ya dau la pauni milioni 15 ili kumnunua winga wa Burnley wa chini ya umri wa miaka 21, Dwight McNeil. **(Football Insider)**

**LEICESTER YAMTAKA EDOUARD**
KLABU ya Leicester City ina imani ya kuzipiku Liverpool na West Ham United katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Celtic, Odsonne Edouard mwenye umri wa miaka 23. **(Teamtalk)**

**WIJNALDUM AITAKA BAYERN**
WAKALA wa Georginio Wijnaldum wamesema kiungo huyo wa kati wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 30, angependelea kuzungumza na Bayern Munich kuhusu uhamisho wa bure baada ya mkataba wake kumalizika kule Liverpool msimu huu. **(Sport1)**

**ONANA ATAKIWA GUNNERS**
ARSENAL wanatathmini uwezekano wa kumnunua kipa wa Ajax na Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 25. **(Goal)**

**WEST HAM, SPURS KWA LARIN**
TOTTENHAM Hotspur na West Ham ni miongoni mwa klabu za Ulaya zinazomfuatilia mshambuliaji wa Besiktas na Canada, Cyle Larin mwenye umri wa miaka 26. **(90Min)**



HABARI MICHEZO

# TALIB AIONYA TIMU YA TAIFA YA UFUKWENI KWA SENEGAL

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya soka la Ufukweni nchini Oman, Talib Hilal, ameangalia wapinzani wa Tanzania na kisha kusema "msiwachukulie poa Senegal" katika michuano ya Fainali ya Mataifa ya Afrika.

Tanzania imepangwa na timu ya Senegal, DR Congo na Uganda katika michuano hiyo inayotarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi huu, huku Senegal wakiwa wenyeji wa mashindano hayo.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Talib Hilal, alisema kwa timu zilizopangwa na Tanzania mechi dhidi ya Senegal itakuwa ngumu kutokana na uzoefu wa nchi hiyo katika mashindano hayo huku pia ikiwa imewahi kucheza Kombe la Dunia.**

Alisema Senegal pia itakuwa inabebwa na uwenyeji wa michuano hiyo na kuhusu Uganda na Congo ana matumaini Tanzania inaweza kufanya vizuri kama itajiandaa vema.

"Kwa Tanzania mechi ngumu ni dhidi ya Senegal, kwanza ni wenyeji wa mashindano, pili mara nyingi wameshiriki Kombe la Dunia, wanatakiwa kujitahidi wasiwape nafasi Senegal kupiga mashuti, wacheze kwa kujiamini na wasiwaogope," alishauri Talib.

Alisema Uganda na Congo ni mara ya kwanza kushiriki wakati Tanzania hii ni mara ya pili, hivyo anaipa nafasi kubwa kufika nusu fainali na cha muhimu kwa sasa ni kufanya maandalizi kama mazuri.

Tanzania inaendelea na mazoezi yao katika fukwe za Coco kujiandaa na michuano hiyo chini ya Kocha Mkuu, Boniface Pawasa, ambapo inatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya timu ya Ufukwe kutoka Zanzibar kabla ya kwenda Senegal kushiriki michuano hiyo.

## MANARA AWAANGUKIA MASHABIKI WA SIMBA

**Na Mwandishi Wetu**

PAMOJA na juhudi zake za kuhamasisha mashabiki kujitokeza kwa wingi kuishangilia timu yao dhidi ya Yanga Jumamosi, Ofisa Habari wa Simba, amelazimika kuwaangukia kwa kuwaomba radhi kutokana na kutii wito huo, lakini mechi ikishindwa kuchezeka.

Mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara iliyokuwa ipigwe Uwanja wa Benjamin Mkapa majira saa 11:00 jioni, ilivunjika kutokana na timu ya Yanga kugomea mabadiliko ya muda baada ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kueleza kupokea maagizo kutoka serikalini yakitaka mchezo huo usogezwe mbele hadi saa 1:00 usiku.

Yanga iligomea uamuzi huku ikidai kuwa ni kinyume cha Kanuni ya 15 (10) ya Ligi Kuu inayohusu taratibu za michezo ambayo inataka mabadiliko yote ya michezo kujulishwa kwa pande zote husika angalau saa 24 kabla ya muda wa awali.

Lakini Manara ambaye kwa muda wiki nzima kuanzia Jumatatu iliyopita alizunguka kwenye vituo vya redio, televisheni na magazeti mbalimbali kufanya promosheni kubwa kuelekea mchezo huo ambao baadaye uliahirishwa, amesikitikia hatua hiyo huku akiwaomba msamaha.

"Sijilaumu kwa kile nilichofanya kwa niaba ya klabu yangu, lakini nimeumizwa sana kuona mashabiki wake hawakupata walichokitarajia, najihisi ni mkosaji na nadhani kuna haja ya kuwajibika kwa kitendo kile.

"Nilitumia nguvu kubwa kuhakikisha tunajaza uwanja, lakini matokeo yake ni maumivu yaliyoacha doa kuu. Nawaza kwa hisia, kwa nini sauti yangu iwe sehemu ya kuwapa maumivu wengine? Wangapi wamejeruhiwa kimwili na kiakili kwa kilichotokea jana?" Manara alihoji.

Alisema anaogopa na naomba msamaha kwa mashabiki wote hususan waliojitokeza kwa Mkapa kushuhudia mechi hiyo ambayo hata hivyo haikufanyika.

"Binafsi nipo katika kipindi kigumu mno, kila nikiwafikiria mashabiki wale ambao 'always' [mara zote] ndio huufanya mchezo huu wa soka kuwa hivi ulivyo sasa.

"Inawezekana nisiwe nahusika hata kidogo kuahirishwa kwa mchezo ule, lakini nitakuwa mpuuzi nisiposema samahani kwenu, imani yangu taarifa rasmi ya klabu juu ya kadhia hii nzito itatolewa," alisema.




Wachezaji wa Simba wakiwaaga mashabiki katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, baada ya kuahirishwa kwa mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Yanga kutokana na watani wao hao kugomea mchezo huo kuchezwa saa 1:00 usiku badala ya saa 11:00 jioni. PICHA: JUMANNE JUMA

# Yanga: Simba washukuru kuepuka kipigo

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kugoma kucheza mechi ya watani wa jadi dhidi ya Simba baada ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kusogeza mbele muda wa mchezo huo juzi, Jumamosi, uongozi wa Yanga umesema "wanabahati hao wangekula nyingi".

Mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara mzunguko wa pili, ilikuwa ichezwe saa 11:00 jioni katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, lakini zikiwa zimebaki saa tatu kabla ya mchezo huo kuanza, TFF ilizitaarifu klabu zote mbili kuwa imepokea maagizo kutoka serikalini kupitia wizara husika ya michezo kuwa mechi hiyo isogezwe mbele na kuchezwa saa 1:00 usiku.

Hata hivyo, Yanga iligomea uamuzi huku ikidai kuwa ni kinyume cha Kanuni ya 15 (10) ya Ligi Kuu inayohusu taratibu za michezo ambayo inataka mabadiliko yote ya michezo kujulishwa kwa pande zote husika angalau saa 24 kabla ya muda wa awali.

Kutokana na kauli hiyo Yanga walipeleka timu saa 10:20 jioni kisha wakafanya mazoezi na kuondoka jumla saa 11:39 huku wakipishana na Simba ambao waliingia saa 11:27.

Lakini baada ya kuondoka uwanjani hapo kupitia ukurasa wao wa mtandao ya kijamii wa Instagram, Yanga iliwashukuru mashabiki na wanachama ambao walijitokeza kwa wingi Uwanja wa Mkapa kwa ajili ya mchezo huo dhidi ya Simba na kusema kuwa wana bahati wapinzani wao wangefungwa nyingi. "Shukran kwa mashabiki, wanachama na wapenzi wa Young African SC kwa kujitokeza kwa wingi Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mchezo wetu dhidi ya Simba.

"Bahati yao maana walikuwa wanakufa nyingi, tulieni Wananchi, haki inaweza kucheleweshwa, lakini haiwezi kupotea," ilieleza klabu hiyo.

Tayari TFF, imeeleza katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari kuwa itakutana na klabu hizo mbili kulishughulikia suala hilo kikanuni.

Michezo
Jumatatu Mei 10, 2021
Nipashe



HAALAND SASA SOKONI KWA PAUNI MILIONI 150

HABARI UK 22

SUBIRINI...



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini, timu hiyo inatarajiwa kuelekea Afrika Kusini leo kwa ajili ya mechi yao ya robo fainali ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Kaizer Chiefs Jumamosi. **PICHA: MAKTABA YETU**

# GOMES: HASIRA YANGA SASA KWA KAIZER CHIEFS

●●●Alia mashabiki kuikosa burudani kwa Mkapa, lakini awaahidi furaha Jumamosi kwenye...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

BAADA ya Bodi ya Ligi Tanzania Bara kuahirisha mchezo kati ya Simba dhidi ya Yanga, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema walipata mshtuko kutokana na taarifa hizo kwa sababu aliandaa kikosi chake kwa ajili ya kuvuna pointi zote tatu katika mchezo huo uliokuwa upigwe Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara mzunguko wa pili, ilikuwa ichezwe saa 11:00 jioni lakini zikiwa zimebaki saa tatu kabla ya mchezo huo kuanza, TFF ilizitaarifu klabu zote mbili kuwa imepokea maagizo kutoka serikalini kupitia wizara husika ya michezo kuwa mechi hiyo isogezwe mbele na kuchezwa saa 1:00 usiku.

Hata hivyo, Yanga iligomea uamuzi huo kuwa ni kinyume cha Kanuni ya 15 (10) ya Ligi Kuu inayohusu taratibu za michezo ambayo inataka mabadiliko yote ya michezo kujulishwa kwa pande zote husika angalau saa 24 kabla ya muda wa awali.

Lakini Gomes akizungumza na gazeti hili jijini jana, alisema walijipanga vizuri kwa ajili ya kuvuna pointi zote tatu ila wameshtushwa na kilichotokea kwa kuwa wote walipokea taarifa muda mmoja, hivyo maandalizi hayo anayageuzia kwa Kaizer Chiefs Jumamosi.

Alisema hawakuwa na namna kwao hasa baada ya kupata taarifa za kusogezwa mbele kwa muda, lakini kikubwa ilikuwa ni jinsi walivyojiandaa.

"Nina imani tulijiandaa vizuri na tulikuja kutafuta pointi tatu, haya mambo mengine ya kubadilisha muda hatuwezi kuona shida kwa sababu hakuna namna, inategemea na jinsi ya timu ilivyojiandaa," alisema Gomes.

Alisema kwa maandalizi waliyoyafanya ana imani mchezo ungekuwa mzuri na mashabiki wao wangepata burudani kutokana na kandanda safi la kuvutia ambalo wangelitandaza.

Aidha, Gomes alisema amesikitikia mashabiki waliojitokeza Uwanja wa Benjamin Mkapa kuangalia mechi hiyo ya watani wa jadi lakini wakashindwa kupata burudani hiyo, wakiondoka nyumbani patupu.

"Unaweza kusema kwamba ni huzuni na masikitiko kuona mashabiki ambao wamejitokeza kutazama burudani, lakini haijawa hivyo. Hamna namna kwetu. Imekuwa ni mshtuko kwa kilichotokea kwa sababu tayari tulikuwa tumejiandaa kwa ajili ya mechi hii," alisema. Kocha huyo alisema sasa akili na nguvu zao ni kwa ajili ya maandalizi ya mechi yao dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini kwenye mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema mipango yake ilikuwa mechi dhidi ya Yanga kuwa sehemu yao ya maandalizi ya mchezo wao wa robo fainali ya michuano hiyi mikubwa Afrika kwa ngazi ya klabu.

"Ni mechi ya ushindani mkubwa, si rahisi mchezo dhidi ya Yanga ilikuwa ni moja ya maandalizi yetu kuelekea mechi hiyo ya michuano ya kimataifa ambayo tunatarajia kucheza hivi karibuni," alisema Gomes.

Alisema wanatarajia kuondoka nchini leo kuelekea Afrika Kusini kwa ajili ya mechi hiyo.

"Tunaanzia ugenini, ni mchezo muhimu, wachezaji wanajua umuhimu wa mchezo huo hivyo tunahitaji kwenda kutafuta matokeo chanya ili kuendelea kujiimarisha kwenye safari yetu ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Gomes.

## TFF YAOMBA RADHI MASHABIKI, WADAU

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeomba radhi kwa wadau wa soka baada ya kutofanyika kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya watani wa jadi, Simba na Yanga uliokuwa upigwe Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi.

Taarifa ya TFF jana ilieleza kuwa tayari imeitaka Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) kutoa taarifa ya kina kuhusu kuahirishwa kwa mchezo huo pamoja na kushughulikia hatima ya wapenzi wa soka waliolipa viingilio kuingia uwanjani.

"Tunawaomba wapenzi wa mpira wa miguu kuwa watulivu wakati jambo hili linashughulikiwa kwa haraka kwa taratibu za kikanuni, lakini huku tukishirikiana kwa karibu na wadau wote ikiwamo serikali," ilieleza taarifa ya TFF kupitia kwa Ofisa Habari wake, Cliford Ndimbo.

Juzi saa 8:33 mchana TFF ilitoa taarifa ya kusogeza mbele mechi kutoka saa 11:00 jioni hadi saa 1:00 usiku, ikisema imepokea maagizo kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kufanya hivyo, hata hivyo haikutaja sababu.

Hata hivyo, Yanga iligomea uamuzi huo kuwa ni kinyume cha Kanuni ya 15 (10) ya Ligi Kuu inayohusu taratibu za michezo ambayo inataka mabadiliko yote ya michezo kujulishwa kwa pande zote husika angalau saa 24 kabla ya muda wa awali.

Hivyo, Yanga ikawasili uwanjani hapo saa 9:30 na kufanya mazoezi ya kupasha misuli kabla ya kurejea vyumbani kusubiri muda wa kuitwa na waamuzi kuingia uwanjani, lakini saa 11:30 wakaondoka kurejea kambini kwao.

Baadaye Simba nao wakaingia uwanjani kufanya mazoezi pia kabla ya kurejea vyumbani na kisha nao kuondoka baada ya kutangaziwa kuwa mechi hiyo imeahirishwa.

Maelfu ya mashabiki waliobaki uwanjani walianzisha vurugu kudai warejeshewe viingilio, kabla ya Jeshi la Polisi kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002